
TNP/BDS/B/01

# HIFADHI ZA TAIFA Tanzania



Kiswahili

2020/1

Rev.0:Jan. 2023



TANZANIA
Usiyoweza Kuisahau!

# Karibu katika dunia yetu!

au kama vile wenyeji wasemavyo, "Karibu sana". Watanzania ni miongoni mwa watu wenye upendo na wakarimu sana duniani. Karibu Hifadhi za Taifa Tanzania; dunia yenye wanyamapori na uzuri usio na ushindani duniani kote.

Kwetu sisi hii ni safari endelevu ya uhifadhi na utunzaji wa maeneo yenye mapori pamoja na aina mbalimbali za wanyamapori wa ajabu. Maeneo ishirini na mbili kati ya hayo kwa sasa yanaangaliwa na si tu kwa faida yetu bali kwa furaha ya binadamu wote.

Hili ni jambo ambalo tunajivunia sana, na tunakualika wewe mgeni wetu mpendwa upate kufurahia uzuri na maajabu haya.


| | |
|---|---|
| Hifadhi ya Taifa Arusha | 2 |
| Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato | 4 |
| Hifadhi ya Taifa Gombe | 6 |
| Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa | 8 |
| Hifadhi ya Taifa Katavi | 10 |
| Hifadhi ya Taifa Kigosi | 12 |
| Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro | 14 |
| Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane | 16 |
| Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo | 18 |
| Hifadhi ya Taifa Kitulo | 20 |
| Hifadhi ya Taifa Mikumi | 22 |
| Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale | 24 |
| Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa | 26 |
| Hifadhi ya Taifa Mkomazi | 28 |
| Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla | 30 |
| Hifadhi ya Taifa Nyerere | 32 |
| Hifadhi ya Taifa Ruaha | 34 |
| Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe | 36 |
| Hifadhi ya Taifa Saadani | 38 |
| Hifadhi ya Taifa Serengeti | 40 |
| Hifadhi ya Taifa Tarangire | 42 |
| Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara | 44 |
| Ilani ya Arusha | 46 |
| Wajibu wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa | 46 |
| Wito wa Afrika | 49 |
| Historia fupi ya TANAPA | 50 |
| Tozo za Hifadhi | 52 |



# Uzuri wa Hifadhi Zetu

**Hakuna safari ya kitalii inayosisimua na kufurahisha unayoweza kuilinganisha na safari halisi ya kutalii katika Hifadhi za Taifa.** Ukiangalia wanyamapori wa aina mbalimbali, mandhari nzuri, mimea, ndege, wadudu, fukwe, milima na vilima vinavyoambatana na huduma bora inayotolewa na wafanyakazi wetu, hakika yote haya yanafurahisha!

Kadiri miaka inavyozidi kwenda hifadhi zetu zinaendelea kuwa bora kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara na malazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Pia hifadhi zetu zimekuwa zikitangazwa na kupata tuzo mbalimbali za kitaifa na kimataifa na kuvutia wageni wengi duniani kuja kutembelea Tanzania.

Hifadhi hizi ni vyanzo vya hewa na maji safi yanayotiririka kwa mwaka mzima. Ukiwa ndani ya hifadhi unaweza kuona vivutio kwa kutumia magari wakati wa mchana au usiku, kutembea kwa miguu, kupanda puto, kuruka na parashuti, kuendesha baiskeli, kutembea juu ya daraja la kamba, kuendesha boti na mitumbwi, kula chakula cha moto porini na kupanda milima. Hifadhi zetu zina makundi makubwa ya mamalia ambao wamesalia duniani, wingi na ubora huu wa wanyamapori unatokana na juhudi kubwa ya ulinzi na usimamizi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Kipeperushi hiki ni utangulizi wa taarifa kuhusiana na Hifadhi za Taifa ambacho kinalenga kukupatia taarifa muhimu za kukuwezesha kuanza kupanga safari yako ya kutalii na kufurahia vivutio vingi vinavyo patikana katika maeneo tunayo yahifadhi. Tunawakaribisha wageni wote kuja kutembelea Hifadhi za Taifa ili kujifunza masuala ya wanyamapori na mazingira, kufurahia na kupiga picha za ukumbusho.

Tunakukaribisha kutembelea hifadhi zetu na pindi urejeapo usisahau kusimulia yale mazuri uliyoyaona na kuwahamasisha wengine kuja kujionea vivutio na kushiriki katika Uhifadhi kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

.

William S. Mwakilema
Kamishna wa Uhifadhi



# HIFADHI YA TAIFA ARUSHA



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ilianzishwa mwaka 1960 ikiitwa hifadhi ya Taifa Ngurdoto, baadae ilibadilishwa jina na kuitwa Hifadhi ya Taifa Arusha ikiwa na ukubwa wa Kilomita za mraba 322. Kwa sasa hifadhi hii ina ukubwa wa kilomita za mraba 552. Hifadhi hii inasifika kwa uwepo wa mlima Meru, msitu wa kimlima, uwepo wa Mbega wengi, kasoko na maziwa ya Momela.

## Mahali ilipo

Hifadhi ipo Kaskazini mwa Tanzania katika mkoa wa Arusha, ikizungukwa na wilaya za Arumeru, Longido na Arusha.

## Hali ya hewa

Hifadhi hii inaweza kutembelewa kwa kipindi chote cha mwaka japokuwa wakati mzuri zaidi wa kutembelea hifadhi hii ni kuanzia mwezi Juni hadi Oktoba na kuanzia Desemba hadi mwanzoni mwa mwezi Machi. Kipindi cha mvua za muda mfupi huanza mwezi Oktoba hadi Novemba na kipindi cha mvua nyingi ni kuanzia mwezi Machi hadi Mei.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara.

**Kwa barabara:** Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara kilomita 32 kutoka jiji la Arusha na kilomita 40 kutoka uwanja wa ndege wa kimaTaifa wa Kilimanjaro.

## Vivutio vya Utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi hii ina aina mbalimbali za mamalia ikijumuisha Twiga, Tembo, Chui, Tumbili, Funo, Kulungu, Mbega weupe, Nyani, Nyati, Kuro na Viboko. Kuna zaidi ya aina 450 za ndege zilizoainishwa.
- **Mlima Meru;** Mlima Meru una volkano iliyolala yenye umri wa takribani miaka milioni moja na nusu (1.5 milioni) iliyopita. Mlipuko wa volkano ulisababisha maporomoko makubwa ya matope na miamba na kutengeneza milima, mabonde na maziwa madogo.
- **Maporomoko ya maji;** Tululusia na Maio ni maporomoko makubwa yanayopatikana katika hifadhi hii na ni kivutio kikubwa kwa wageni wanaokuja kutembelea hifadhi.
- **Ziwa Momella kubwa na Momella ndogo;** Maziwa haya hupokea maji ya mito ipitayo chini ya ardhi na hayana kina kirefu. Kutokana na kuwa na aina tofauti ya alkali, kila ziwa lina aina tofauti ya algae hivyo kuyapa maziwa haya muonekano wa rangi tofauti.
- **Ziwa la Longil;** Hili ndio ziwa pekee katika hifadhi lenye maji yasiyo na chumvi ambapo samaki aina ya Tilapia (perege) hupatikana ikiwa ni pamoja na mimea aina ya Mafunjo (Papyrus) na Matete (Mace) ambayo huonekana kama visiwa na uhama kulingana na mwelekeo wa upepo.
- **Msitu wa Ngurdoto;** Msitu huu wa kimlima una mvuto wa kipekee kwani ni makazi ya wanyama na ndege wengi wa msituni.
- **Serengeti Ndogo;** Hii ni mbuga ya wazi inayofanana na mbuga zinazopatikana katika hifadhi ya Taifa Serengeti ambapo aina mbalimbali za wanyama kama Ngiri, Pundamilia, Kuro, Twiga, Pongo na Mbogo hupatikana kwa wingi.





- **Uwanja wa mbogo;** Hili ni eneo la wazi lenye vichaka na nyasi fupi ambazo huvutia wanyama kama Nyati, Ngiri na Twiga.
- **Kasoko ya Ngurdoto na Meru;** Kasoko hizi ni kivutio kizuri kwa utalii kwani unapokuwa kwenye maeneo haya unapata fursa ya kuona mlima Kilimanjaro uliofunikwa kwa barafu, maziwa ya momella na ukanda wa chini wenye makazi wa watu.
- **Mti wa Lango (Mkuyu);** Mti huu uliota na kuwa na pango kubwa katikati na magari madogo au mnyama kama tembo anaweza kupita.
- **Mto Ngarenanyuki;** Mto huu ambao chanzo chake ni msitu mnene wa mlima na kasoko ya Meru, una maji yenye kufanana na chai ya rangi ya kiafrika ambayo inasababishwa na uwepo wa mchanganyiko wa madini kutoka kwenye vijito viunavyounda mto Ngarenanyuki

## Shughuli

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja

- Utalii wa kutwa wa kuona wanyama kwa kutumia magari;
- Utalii wa kutembea kwa miguu. Hifadhi ya Taifa ya Arusha ni maarufu kwa utalii wa kutembea kwa miguu. Pia ni eneo ambalo unaweza kufurahia misitu ya asili kwa sababu ya hali ya hewa yenye joto na baridi ya kadiri;
- Utalii wa kupanda Mlima. Haya ni matembezi ya siku nne kuelekea kilele cha mlima Meru. Matembezi haya yanatakiwa kuandaliwa mapema kwa kushirikisha wakala wa utalii;
- Utalii wa kupiga kasia. Utalii huu wa kupiga makasia kwa kutumia mitumbwi hufanyika kwenye ziwa momella ambapo mgeni anapata fursa ya kujionea ndegemaji na wanyama waishio majini;
- Utalii wa kupanda farasi. Utalii huu ni wa kipekee kabisa unaofanywa hifadhini. Mtalii anayefanya utalii huu anakuwa na fursa ya kuwasogelea wanyama kwa ukaribu zaidi kwani wanyama hawakimbii kutokana na kwamba farasi nae ni mnyama; na
- Utalii wa kuendesha baiskeli. Utalii huu hufanyika kuanzia lango la Ngongongare kupitia msitu wa kilinga, mzunguko wa Mbega hadi lango la Momela. Utalii huu unatoa fursa kwa mgeni kuwepo kwenye mazingira asilia ya nyika na pori.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi:** Kambi za kupiga hema za jumuia na binafsi. Pia zipo nyumba za kupumzikia wageni na koteji za kulala wageni mlimani.

Pia zipo loji zinazomilikiwa na watu binafsi ndani ya hifadhi ambapo taarifa za awali zinahitajika kabla ya kuja kwa ajili ya kulala.

**Nje ya hifadhi**: Zipo hoteli nyingi nje ya hifadhi katika mji mdogo wa Usa river, Mji wa Moshi - Kilimanjaro na Jiji la Arusha.

**Mawasiliano**

Simu: +255 272 553 696
Barua pepe: arusha@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 689 062 363
Instagram: arusha_nationalpark

## HIFADHI YA TAIFA

# BURIGI-CHATO



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato ilipandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2019. Hifadhi hii ni muunganiko wa mapori ya akiba matatu ambayo ni Burigi, Biharamulo na Kimisi yaliyoanzishwa rasmi mnamo mwaka 1970. Hifadhi ina ukubwa wa kilomita za mraba 4,707. Hifadhi ina eneo kubwa la mbuga lenye maziwa yenye maji baridi, milima, miinuko yenye miamba, mabonde marefu yenye misitu, nyanda zenye uwazi, vinamasi, mito na nyanda zenye miti ya savana aina ya Miombo. Jambo kubwa la kuvutia katika Hifadhi hii ni maziwa yaliyopo huku Ziwa Burigi likiwa ni ziwa kubwa ambalo linatoa fursa nzuri kwa ajili ya kuendesha mtumbwi na kufurahia michezo ya kwenye maji.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato ipo katika mikoa miwili ya Kagera na Geita, kwenye wilaya za Ngara, Karagwe, Biharamulo, Muleba na Chato.

## Hali ya Hewa

Hifadhi ipo kwenye eneo lenye misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambapo mvua za muda mfupi huanza kunyesha mwezi Novemba hadi Desemba na mvua za muda mrefu (masika) huanza kunyesha mwezi Machi hadi Aprili.



Kipindi cha kiangazi ni kuanzia mwezi Juni na kuishia Septemba na kuambatana na joto la wastani wakati wa mchana na hali ya baridi ya wastani nyakati za usiku. Aidha, muda mzuri wa kutembelea hifadhi ni kuanzia mwezi Juni hadi Oktoba na Januari hadi Machi.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara:** Hifadhi inaweza kufikika kutoka Chato mjini hadi lango la Katete umbali wa kilomita 40. Pia malango mengine ya hifadhi yanafikika kwa barabara ambapo lango la Kijuu kutoka Muleba ni kilomita 80, lango la Nyungwe kutoka Ngara ni kilomita 70 na Rusumo ni kilomita 47; lango la Ruhita kutoka mpaka wa Mutukula ni kilomita 150.

**Kwa anga:** Hifadhi inafikika kwa njia ya anga kupitia uwanja wa ndege wa kimaTaifa wa Geita uliopo wilaya ya Chato umbali wa kilomita 40. Zipo ndege





za kukodi ambazo zitakufikisha hadi kwenye kiwanja kidogo cha Nkonje kilichopo hifadhini. Viwanja vingine vya karibu ni pamoja na Biharamulo na Bukoba.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi ina aina mbalimbali za wanyama ikiwa ni pamoja na Pofu, Tembo, Simba, Nyati, Swala Pala, Palahala, Chui, Pundamilia, Twiga, Fisi madoa, Nyamera, Pongo, Dikidiki, Tohe, Kuro na Oribi.
- **Ndege;** Hifadhi ina jamii mbalimbali za ndege wahamao na wale wasiohama wakijumisha ndege wa asili akiwemo Domo Kiatu aliye hatarini kutoweka. Pia kuna ndege aina ya Kwezi anayeonekana kwa urahisi wakati wa kufanya utalii wa boti.
- **Uoto wa Asili;** Mazingira ya hifadhi yanapambwa na maeneo ya wazi yenye nyasi fupi, yakiungana na misitu mchanganyiko, vichaka, uoto wa miti ya migunga inayotoa makazi kwa wanyama aina ya Twiga. Mandhari ya kuvutia inayotokana na miti jamii ya Miombo ambayo ni makazi kwa wanyama jamii za Nyani, Chui na wengineo.
- **Kuwepo kwa Maziwa Mazuri;** Uzuri wa hifadhi unakamilishwa na maziwa matano yenye mwonekano wa kipekee ya Victoria, Nyarwambaire, Kasinga, Burigi na Ngoma.
- **Mto Kagera;** Kwa upande wa Magharibi hifadhi imetenganishwa na nchi jirani ya Rwanda kwa Mto Kagera unaoambaa pembezoni mwa hifadhi.

## Shughuli za Utalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kuona wanyama kwa kutumia gari;
- Kutembea kwa miguu na kujionea wanyama;
- Kuangalia ndege wa msituni na ndegemaji;
- Kurekodi filamu;
- Utalii wa kuangalia nyota; Ukiwa umepiga kambi huku umejipumzisha eneo la wazi, utaweza kuangalia anga lililopambwa na nyota nyingi wakati wa usiku; na
- Utalii wa kupiga Kasia; Aina hii ya utalii unakupa fursa ya kufurahia fukwe za asili za ziwa Burigi, kuona wanyama na ndegemaji.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi:** Kuna maeneo ya kupiga mahema na nyumba za kualala wageni zinazomilikiwa na hifadhi.

**Nje ya hifadhi:** Kuna nyumba za kulala wageni katika wilaya za Biharamulo, Muleba , Chato, Ngara, Karagwe, Geita na Bukoba.

**Mawasiliano**
Simu: +255 282 983 204
Barua pepe: bc@tanzaniapark.go.tz
Instagram: burigichato_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# GOMBE



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Gombe ilipandishwa hadhi na kuwa hifadhi ya Taifa mwaka 1968 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 35. Kabla ya kupandishwa kwake eneo hili lilitambuliwa kwa mara ya kwanza kama hifadhi muhimu ya wanyamapori na makazi ya Sokwemtu mwaka 1943 ambapo ilipewa hadhi ya kuwa pori la akiba Gombe. Mnamo Juni 2013, Serikali kupitia tangazo la gazeti la Serikali Namba 228 liliongeza eneo la ziwa Tanganyika lenye ukubwa wa kilomita za mraba 21.2 katika eneo la Hifadhi ya Taifa Gombe,na kufanya hifadhi hii kuwa na jumla ya kilomita za mraba 56.2. Hifadhi hii ni miongoni mwa makazi machache yaliyosalia ya Sokwemtu duniani, mnyama anayeitambulisha hifadhi hii na kuwavutia wageni wengi. Sokwe mtu hawa wamefanyiwa utafiti wa muda mrefu na mwanasayansi na mtunza mazingira na viumbe hai maarufu ajulikanaye kama Dr. Jane Goodall.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Gombe ipo katika mkoa wa Kigoma, Kaskazini mwa mji wa Kigoma-Ujiji pembezoni mwa Ziwa Tanganyika.

## Hali ya hewa

Hifadhi hupata mvua mara mbili kwa mwaka, ambapo mvua za vuli hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Desemba na masika kuanzia mwezi Machi hadi Mei. Kiangazi huanza mwishoni mwa mwezi Juni hadi Oktoba na pia kuanzia Januari hadi Machi.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya maji kwa kutumia boti za kukodi kutoka mji wa Kigoma.

Unaweza kufika Kigoma kwa njia ya barabara, treni na anga:-

**Kwa barabara;** Unaweza kufika mkoa wa Kigoma kwa njia ya barabara kutoka miji na majiji yote makubwa nchini. Kutoka Kigoma utatumia usafiri wa boti za kukodi kwenda hifadhini.

**Kwa treni;** Unaweza kufika mkoa wa Kigoma kwa kutumia reli ya kati na kukodi boti hadi hifadhini.

**Kwa anga;** Unaweza kufika mkoa wa Kigoma kwa kutumia usafiri wa ndege na kutua uwanja wa ndege wa Kigoma na kukodi boti hadi hifadhini.



## Vivutio Vya Utalii

- **Sokwemtu;** Sokwe ni kivutio kikuu hasa kwa kuwa wanatabia zinazokaribiana sana na binadamu na wanasayansi wamegundua kuwa vinasaba vyao vinafanana na binadamu kwa zaidi ya asilimia 98. Tabia za mikusanyiko yao, michezo, milio, utafutaji wa chakula na mahusiano mengine katika makundi vinaelezea ni jinsi gani Sokwe hao wanakaribiana sana na binadamu.
- **Wanyamapori;** Kuna zaidi ya aina 35 za mamalia zinazopatikana katika hifadhi hii ikijumuisha Tumbili, Nyani, Kima, Nguruwepori, Pongo, Kenge, Nyoka na ndege.
- **Ziwa Tanganyika;** Ziwa Tanganyika ni kivutio kikubwa hasa kwa kuwa ni ziwa la pili kwa kuwa na kina kirefu duniani kiasi cha mita 1,447.
- **Samaki wa kipekee;** Ziwa hili lina zaidi ya aina 300 za samaki na wengi wao hawapatikani katika maeneo mengine kama Kuhe na Mgebuka.
- **Mandhari nzuri;** Mandhari ya Gombe ni nzuri mno yenye zaidi ya mabonde makuu 16 yenye vijito viendavyo kasi, ambavyo hutiririka maji mwaka mzima.
- **Kingo za Milima;** Hifadhi ina kingo za milima na mabonde ambapo ndipo maeneo unayoweza kuwaona Sokwemtu ukiwa unatembea kwa miguu.

## Shughuli za Utalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Kuangalia Sokwemtu. Matembezi ya kuongozwa ndani ya msitu kuwangalia na kukaa na Sokwemtu hawa ni kivutio kikubwa kwa watalii. Gombe ina idadi kubwa ya Sokwemtu ukilinganisha na ukubwa wa eneo. Utaweza kuanza safari yako ya kwenda kuwaona Sokwemtu kuanzia kwenye fukwe za mchanga wa ziwa Tanganyika;
- Utalii wa kupiga picha za filamu. Mandhari ya hifadhi hii ambayo ni mabonde yaliyofunikwa na msitu mnene unaokutana na fukwe za ziwa Tanganyika huwawezesha wageni kupata picha za kutengeneza filamu nzuri za Sokwemtu;
- Kutazama Ndege. Zaidi ya aina 200 za ndege hupatikana katika eneo hili wengi wao wakiwa ndege wa msituni na ndegemaji. Kipindi cha mvua ndegemaji wengi huonekana wakizunguka ziwani kutafuta samaki;
- Kupanda Milima. Utalii wa kupanda na kushuka kwenye vilele vya milima huku ukifurahia kuona msitu, mito, maporomoko ya maji, Sokwemtu, wadudu, ndege na wanyama wengine;
- Michezo ya kwenye maji. Utalii huu wa kuogelea na kuzama kwenye maji ya Ziwa Tanganyika hutoa burudani ya kipekee kwa wageni; na
- Utalii wa boti. Utalii wa kutumia boti ya kifahari au boti iendayo kwa kasi unakupa nafasi ya kujionea Wanyama mbalimbali wa ziwani na pia kuweza kutembelea vijiji vilivyo karibu na kujionea tamaduni mbalimbali za wakazi wa maeneo haya.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi:** Nyumba moja ya kulala (Koteji) katika eneo la Mtumba na Kasekela na sehemu ya kupiga mahema iliyopo eneo la utalii Kasekela.
**Nje ya hifadhi:** Kuna nyumba za kulala wageni za aina na viwango mbalimbali katika mji wa Kigoma.

**Mawasiliano:**

| | |
|---|---|
| Simu: | +255  282 988 228/229 |
| Barua pepe: | chimps@tanzaniaparks.go.tz |
| Whatsapp: | +255 689 062 303 |
| Instagram: | gombe.nationalpark |

# HIFADHI YA TAIFA
# IBANDA-KYERWA



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa ilipandishwa hadhi kutoka pori la akiba kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2019 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 294. Hifadhi ni maarufu kwa chemichemi za maji za kudumu pamoja na mto Kagera unaotiririsha maji yake hifadhini. Hifadhi hii iliyopambwa na mikunjo ya milima, mabonde, tambarare, mito ya muda na kudumu, ardhi oevu na vinamasi, vyote hivi vinaifanya hifadhi kuwa na madhari nzuri na ya kipekee.

## Mahali ilipo

Hifadhi ipo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania katika Mkoa wa Kagera wilaya ya Kyerwa. Pia ni hifadhi pekee Tanzania inayopakana na nchi mbili ambazo ni Uganda na Rwanda.

## Hali ya hewa

Hifadhi hii ina misimu miwili ya mvua ambapo mvua za vuli huanza mwezi Oktoba hadi Novemba na msimu wa masika huanza mwezi Machi hadi Mei. Msimu wa kiangazi ni kuanzia mwezi Juni hadi Octoba na Januari hadi Februari.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga;

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kutoka mji wa Bukoba hadi Murongo kilomita 221 au Chato hadi Murongo kilomita 441. Pia hifadhi inafikika kutokea Uganda kupitia mpaka wa kimaTaifa wa Murongo ambapo ni kilomita 4 toka makao makuu ya hifadhi.

**Kwa anga;** Hifadhi inafikika kwa njia ya anga kupitia viwanja vya ndege vya Bukoba na Chato. Pia kwa kutumia ndege ndogo zinazoweza kutua kwenye kiwanja kidogo cha ndege kilichopo katika kijiji cha Ihanda au ndani ya hifadhi.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi hii ina wanyama wa aina mbalimbali kama vile Chui, Nyati, Pofu, Viboko, Korongo, Nyani na Swala wa aina mbalimbali.
- **Mto Kagera;** Mto huu ni moja ya mito mikubwa iliyopo Tanzania ambao pia ni mpaka kati ya Tanzania na Rwanda. Mto huu hutenganisha nchi hizi mbili na pia hifadhi mbili ambazo ni Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa na Hifadhi ya Taifa Akagera ya nchini Rwanda. Pia kwa upande wa Kaskazini mto huu ni mpaka kati ya Uganda na Tanzania.
- **Mandhari nzuri yenye uoto wa asili;** Kuwepo kwa aina nyingi za uoto wa asili kuanzia nyika za miti ya miombo, milima na mabonde, mito na tambarare zinaifanya hifadhi hii iwe na mandhari mazuri ya kuvutia hivyo kuwapa watalii fursa nzuri ya kujionea aina tofauti za uoto wa asili







- **Ndege;** Hifadhi ina ndege wa aina nyingi na wale adimu kama Korongo Nyangumi.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja;

- Utalii wa kutwa wa kuangalia wanyama kwa gari. Utalii wa kuangalia wanyama ni wa kipekee katika hifadhi hii kwani utaweza kujionea wanyama kama vile Chui, Nyati, Pofu, Viboko, Korongo, Nyani na Swala wa aina mbalimbali;
- Matembezi ya miguu. Aina hii ya utalii humwezesha mgeni kuwa karibu zaidi na Wanyama, mimea, ndege na wadudu. Utaweza kujifunza zaidi tabia na maisha ya porini ya Wanyama;
- Utalii wa kuona ndege. Utaweza kuona ndege wa aina nyingi, wahamao na wasiohama kutegemeana na majira ya mwaka; na
- Utalii wa kupiga picha za filamu. Hifadhi hii ina mandhari mazuri kwa ajili ya kupiga picha za filamu kwani maeneo mengi bado yapo katika uasilia wake.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema ya jumuiya na binafsi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji mdogo wa Murongo umbali wa kilomita 3.5 kutoka miji ya Chato au Bukoba.

**Mawasiliano:**

Barua pepe: ibandakyerwa@tanzaniaparks.go.tz
Instagram: ibandakyerwa_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# KATAVI




## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Katavi ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 1974, ikiwa na ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 2,253. Baada ya kutangazwa kwake, eneo lililokuwa pori la akiba la Rukwa liliunganishwa kuwa sehemu ya hifadhi na kufanya eneo la hifadhi kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 4,471. Jina la hifadhi lilitokana na mzimu wa Wabende na Wapimbwe aitwae 'Katabi' ambapo kulingana na wazawa inasemekana mzimu huu ulikuwa unaishi kwenye mti ulio karibu na Ziwa Katavi. Wazawa walikuwa wanatumia eneo hili kuomba baraka na baada ya hapo huacha matoleo yao chini ya mti huu. Hifadhi ya Taifa Katavi ni maarufu kwa wingi wa Viboko na Mamba

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Katavi ipo Kusini Magharibi mwa Tanzania katika mikoa ya Katavi na Rukwa kwenye wilaya ya Tanganyika, Mlele na Mpanda.

## Hali ya hewa

Hifadhi ina msimu mmoja wa mvua ambapo mvua huanza kunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Mei na msimu wa kiangazi ni kuanzia mwezi Juni hadi Oktoba hivyo kuifanya hifadhi ifikike kirahisi kipindi cha kiangazi.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi hii inafikika kwa njia ya barabara, anga na reli.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kwa barabara kutoka Mbeya - Tunduma umbali wa kilometa 520, Kigoma - Mpanda mjini kilometa 362 na Tabora -Mpanda kilometa 375. Kutoka mji wa Mpanda hadi lango la Sitalike kupitia barabara ya Mpanda-Sumbawanga ni kilomita 20.

**Kwa reli;** Unaweza kufika mji wa Mpanda kwa kutumia usafiri wa treni kutokea Mwanza au Dar es Salaam kupitia Tabora.

**Kwa anga;** Hifadhi hii inafikika kwa ndege zinazoweza kutua katika uwanja wa Mpanda. Aidha unaweza kufika Katavi kwa kutumia ndege ndogo za kukodi zinazotua katika viwanja vya Ikuu na Sitalike vilivyopo ndani ya hifadhi.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi ina wingi wa wanyamapori, yapo makundi makubwa ya Nyati, Tembo, Viboko, Pundamilia, Nyamera na swala adimu kama vile Korongo, Palahala na Kongoni. Wanyama wawindao kama Simba na Fisi pia wanapatikana katika maeneo tofauti tofauti. Kuwepo kwa idadi kubwa ya viboko kwenye mabwawa na madimbwi yanayopatikana hifadhini ni kivutio cha kipekee kabisa.




- **Mandhari ya asili;** Mazingira ya asili ambayo bado hayajaharibiwa na binadamu yanayojumuisha tambarare zilizofunikwa na miti ya miombo, vilima, bonde la mlele, mito na misitu yenye wanyama wa aina mbalimbali kunaifanya hifadhi hii kuwa na mandhari ya kipekee.
- **Ndege;** Kuna takribani aina 400 za ndege wanaopatikana katika hifadhi hii. Ndege wanaopatikana kwa wingi zaidi ni pamoja na Kongoti, Korongo Domokijiko, Korongo Domowazi na makundi ya Korongo Domonjano na Korongo Domoganzi. Pia ndege wawindao kama Tai Mlasamaki, Pungu na Tumbusi Mgongomweupe hupatikana kwa wingi.
- **Eneo la kitamaduni;** Hifadhi ina eneo maarufu lenye historia kubwa ya mzimu uitwao "Katabi" na inasemekana kwamba bado mzimu huu upo na kwa wakazi wa eneo hili hutumia mti wa Mkwaju uliopo eneo hili kwa shughuli za kimila na matambiko.

## Shughuli za Utalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja;

- Utalii wa kutwa wa kuangalia wanyama kwa gari. Utalii huu ni wa kuvutia ukiwa ndani ya gari huku ikitazama makundi makubwa ya wanyama kama vile Nyati, Tembo, Viboko na Mamba. Pia wanyama wawindao kama Simba, Chui na Mbwamwitu;
- Utalii wa kutembea kwa miguu. Aina hii ya utalii inakuwezesha kuwa karibu sana na nyika na tambarare za hifadhi. Aina hii ya utalii ni tofauti na ule wa kutumia magari kwani utakuwezesha kujifunza na kuona wanyama wakiwa karibu sana, kuona vitu ambavyo ukiwa ndani ya gari huwezi kuona kama nyayo na wanyama wadogo wadogo;
- Kutazama ndege. Ikiwa na zaidi ya aina 400 za ndege, hifadhi ya Taifa Katavi ni eneo sahihi la kuangalia ndege. Wapo ndege wa aina nyingi kuanzia wale waishio kwenye misitu ya kimto, tambarare, msitu wa miombo na maeneo ya wazi kama vile Tai Mlasamaki, Chole, Chechele Mwekundu, Pungu na Korongo Domongazi. Kwa wapenzi wa ndege usisite kupanga safari yako leo; na
- Mandhari nzuri ya uoto wa asili; Mandhari nzuri ya hifadhi yataipamba safari yako ikiwa ni pamoja na tambarare, nyika za nyasi ndefu na misitu ya miti ya miombo.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi:** Kuna nyumba za wageni zinazomilikiwa na hifadhi (Koteji), kambi za kulala wageni na loji zinazomilikiwa na watu binafsi.

**Nje ya hifadhi:** Kuna aina mbalimbali za malazi katika kijiji cha Sitalike na mji wa Mpanda ambazo zinatoa huduma bora na nzuri.

### Mawasiliano

Simu: +255 767 536 128
Barua pepe: katavi@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 689 062 314
Instagram: katavipark

# HIFADHI YA TAIFA
# KIGOSI



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Kigosi ilipandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2019. Hifadhi hii ni sehemu ya ardhi oevu ya Moyowosi/ Malagarasi ambayo ndiyo ardhi oevu kubwa zaidi Afrika Mashariki. Hifadhi hii ina ukubwa wa kilometa za mraba 7,460.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Kigosi ipo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Kagera na Tabora kwenye wilaya za Ushetu, Bongwe, Bukombe, Biharamulo na Kaliua.

## Hali ya hewa

Hifadhi ina misimu miwili ya mvua ambapo mvua za masika huanza kunyesha kuanzia mwezi Machi hadi Aprili ambapo shughuli kubwa huwa ni kuendesha mitumbwi kwenye vinamasi na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Kutoka Kahama kwenda Hifadhini (Masumbwe) kilomita 57, kutoka Geita hadi Masumbwe kilomita 150.

**Kwa anga;** Kwa kutua katika uwanja wa ndege Kahama.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Wanyama kama Vile Simba, Chui, Fisi, Fisi Maji, Nyati, Kongoni, Nyumbu, Nzohe, Ngiri, Nyani, Pundamilia, Palahala, Pofu, Mbawala, Viboko, Kuro na Mamba huonekana kwa urahisi.
- **Ndege;** Hifadhi hii ni makazi ya aina mbalimbali za ndege wa nchi kavu na ndegemaji ikiwemo ndege adimu kama Korongo-Nyangumi na Korongo -Ndevu. Pia kuna kundi kubwa la bata Bukini Mbilikimo (pengine ambalo ndilo kubwa kuliko yote Afrika).
- **Misitu ya miombo;** Msitu huu umechukua takribani asilimia 60 ya eneo la hifadhi, uoto huu wa misitu ya miombo ni kivutio kizuri kwa watalii wanaotembelea hifadhi.



- **Ardhi oevu;** ardhi ambayo ina uwanda wenye mandhari nzuri ya kuvutia. Una nyanda za pembeni ambazo huwa na mafuriko, zenye miti ya miombo pamoja na michikichi ambazo zinazungunguka maziwa makubwa pamoja na vinamasi ambavyo vingi kati ya hivyo vinabeba visiwa vya mawese na mianzi vinavyoelea.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kuona wanyama kwa kutumia gari;
- Kutembea kwa miguu msituni na kujionea wanyama;
- Kupiga makasia; na
- Kuangalia ndege wa msituni na ndegemaji.

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kambi za kupiga hema za jumuia na binafsi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika miji midogo ya Masumbwe na Kahama.



**Mawasiliano**
Barua pepe: kigosi@tanzaniaparks.go.tz
Instagram: kigosi_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# KILIMANJARO





## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro ilianzishwa mwaka 1973 na kutangazwa na UNESCO (Shirika la Umoja wa MaTaifa la Sayansi na Utamaduni) kuwa Urithi wa Dunia mwaka 1987. Shughuli za utalii zilifunguliwa rasmi mwaka 1977, na mwaka 2013 ilitangazwa kuwa moja ya maajabu saba ya asili Afrika. Hifadhi hii kwa sasa ina ukubwa wa kilomita za mraba 1,668.

## Mahali ilipo

Hifadhi pia inapatikana katika Mikoa miwili ya Kilimanjaro na Arusha kwenye wilaya ya Hai, Longido, Moshi vijijini na Rombo.

## Hali ya hewa

Hifadhi hii ina misimu miwili ya mvua ambapo mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi mwanzoni mwa mwezi Desemba na msimu wa masika huanza mwezi Machi hadi Mei. Msimu wa kiangazi ni kuanzia mwezi Juni hadi Octoba na Januari hadi Februari.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi hii inafikika kwa njia ya barabara, anga na reli;

**Kwa barabara:** Malango yote ya Hifadhi yanafikika kwa njia ya barabara kutokea pande zote za nchi. Lango la Machame lipo umbali wa kilomita 29 kutoka Moshi mjini na lango la Lemosho lipo umbali wa kilomita 56 na lile la Rongai lipo umbali wa kilomita 92. Pia lango la Umbwe lipo umbali wa kilomita 26 kutoka Moshi mjini.

**Kwa anga:** Uwanja wa Ndege wa KimaTaifa wa Kilimanjaro ndicho kituo kikuu cha kufikia wageni wa kimaTaifa na ni kilometa 45 kutoka Moshi mjini.

## Vivutio vya utalii

- Madhari ya Mlima na vilele vyake ambavyo ni Kibo, Mawenzi na Shira;
- Barafu kwenye kilele cha Kibo;
- Wanyamapori na ndege. Kuna uwezekano wa kuona wanyamapori unapotembelea hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, wakiwemo Nyati, Chui, Ngiri, Nguruwe Pori, Mbega, Paa, Tumbili, Kima na Ndege;
- Mimea adimu kama vile ua balsum;
- Mti mrefu kuliko yote barani Afrika;
- Maporomoko ya maji;
- Kasoko ya Maundi;
- Eneo la Matambiko ya wachaga -Kifinika;
- Kilele cha juu kabisa kiliitwa Uhuru baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961.
- Mlima Kilimanjaro ndiyo mlima mrefu kuliko yote Afrika (mita 5,895); na
- Mlima mrefu wa kivolkano uliosimama peke yake duniani.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Kupanda mlima kuelekea kilele cha kibo sehemu ya uhuru;
- Kuendesha baiskeli;
- Kupiga kambi za mahema kawaida na kwenye kasoko;
- Matembezi ya miguu ya kutwa kuona maporomoko ya maji;
- Kuruka kwa parachuti;



- Kupanda miamba kilele cha Mawenzi;
- Mbio za nyika za mlimani; na
- Kupiga picha za filamu.

**Angalizo:** Kuna njia saba (7) za kupanda yaani Londorosi, Lemosho, Machame, Umbwe, Kilema, Marangu na Rongai. Njia iliyokusudiwa kwa lengo la kushuka tu ni Mweka; kupanda na kushuka toka kileleni huchukua siku 5 - 9 au zaidi. Mtalii anayetaka kupanda Mlima Kilimanjaro anashauriwa kupanga safari yake kupitia wakala wa utalii aliyesajiliwa kufanya aina hii ya utalii wa mlima. Nguo za joto na viatu madhubuti vyenye kukinga madhara ya hali ya hewa ni muhimu. Unapopanda unashauriwa kutembea taratibu kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa. Kumbuka methali ya Kiswahili isemayo "Polepole ndio Mwendo"!

## Huduma za malazi

Hifadhi ina huduma maalum za malazi kwenye njia zote za kupanda mlima.

**Ndani ya hifadhi;**

- Kuna hosteli katika lango la marangu.
- Kuna koteji za kulala njia ya Marangu kuanzia kituo cha Mandara hadi Kibo.
- Aidha, njia zingine zilizobaki zina maeneo ya kupiga mahema.

**Nje ya hifadhi;** Kuna malazi ya aina tofauti katika miji ya Moshi, Himo na maeneo yanayouzunguka mlima

### Mawasiliano:

| | |
|---|---|
| Simu: | +255 272 974 153 |
| Barua pepe: | kinapa@tanzaniaparks.go.tz<br>kinapa.tourism@tanzaniaparks.go.tz |
| Whatsapp: | +255 739 767 679 |
| Instagram: | mountkilimanjaro_national_park |



# HIFADHI YA TAIFA
# KISIWA CHA SAANANE




## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2013 kwa kuongeza visiwa vidogo viwili vya Chankende kubwa na Chankende ndogo vilivyopo jirani na maji yanayozunguka hifadhi hivyo kufanya jumla ya ukubwa wa eneo lake kuwa kilometa za mraba 2.18. Hifadhi ni ya kipekee sana Afrika kwani ni Hifadhi ambayo ipo ndani ya mipaka ya jiji. Hifadhi ina wanyama kama vile Simba, Fisi, Swala, Pundamilia, Nyumbu, Mbuzimawe, Pimbi, Tumbili, Digidigi, Fisimaji, Mamba na mchanganyiko wa wanyama wengine. Makazi ya wanyama hawa ni majabali ya mawe, maeneo yenye majani, vichaka vya miiba na miti. Kuna matete ya hapa na pale pamoja na miti mikubwa kuzunguka ufukwe wa kisiwa. Kuna maeneo ya kuangalia mwonekano mzuri wa ziwa na visiwa, hali kadhalika vituo vya kupumzikia, sehemu za kupiga kambi, vibanda vya kupumzikia na mgahawa.





## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane ipo Magharibi mwa Tanzania Mkoa wa Mwanza kwenye wilaya za Ilemela, Nyamagana Misungwi na Sengerema.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua katika Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane ambapo mvua za masika huanza kunyesha kuanzia



mwezi Februari hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, maji na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kwa barabara kupitia jiji la Mwanza ambalo limeunganishwa kwa barabara na reli kutoka maeneo yote ya Tanzania.

**Kwa maji;** Watalii wanaweza kusafiri kwa meli mpaka badari ya Mwanza kutoka Musoma na Bukoba kwa kutumia Ziwa Victoria na pia kutoka Uganda na Kenya.

**Kwa anga;** Hifadhi pia inafikika kwa kutumia uwanja wa ndege wa Mwanza ambao umeunganishwa na miji/majiji yote makubwa ya Tanzania.

## Vivutio vya utalii

- Wanyama mbalimbali kama vile Simba walioko kwenye banda maalum, Pundamilia, Swalapala, Nyumbu, Mbuzi mawe, Kobe na Ndege;
- Jiwe la kuruka;
- Ziwa Victoria;

## Shughuli

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Kutembea kwenye njia mahususi huku ukifurahia mandhari nzuri;
- Kutazama wanyama na ndege;
- Safari za boti;
- Utalii wa kuvua samaki (Uvuaji wa samaki na kuwarudisha tena kwenye maji);
- Kuweka kambi kisiwani; na
- Matukio maalum yanaweza kupangwa kufanyika kisiwani kwenye bustani zilizopo.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi:** Maeneo ya kuweka kambi za jumuia na malazi ya mahema.

**Nje ya hifadhi:** Kuna nyumba za kulala wageni katika jiji la Mwanza.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 282 541 819
Barua pepe: saanane@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 689 062 276 au 0767 536 139
Instagram: saananeisland_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# KISIWA CHA RUBONDO



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ilitangazwa kuwa hifadhi ya Taifa mwaka 1977 ikiwa na eneo la kilomita za mraba 457 ambapo kilomita 236.8 ni nchi kavu na kilomita 220 ni eneo la maji linalozunguka visiwa kumi vinavyoifanya eneo la hifadhi. Ni kisiwa cha tropiki karibu na fukwe za Magharibi za Ziwa Victoria na ni sehemu ambayo haijaharibiwa kabisa. Visiwa hivi vimefunikwa na misitu ya kitropiki ambayo imefanya makazi kwa aina nyingi za wanyama kama Sokwemtu, Tembo na ndege wa aina mbalimbali.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ipo Magharibi mwa Tanzania, katika mikoa ya Geita, Kagera na Mwanza kwenye wilaya za Geita, Chato, Muleba na Sengerema.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za masika huanza kunyesha kuanzia mwezi Februari hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Septemba hadi Novemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Agosti. Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo inaweza kutembelewa nyakati zote za mwaka.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, maji na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kwa barabara kilomita 217 kutoka jiji la Mwanza hadi Mganza.

**Kwa maji;** Mwanza ni jiji la karibu ambapo unaweza kuchukua boti binafsi kwa ajili ya kwenda na kurudi kisiwani.

**Kwa anga;** Kuna uwanja mdogo wa ndege kisiwani na kuna ratiba ya ndege za kawaida kutoka katika miji na majiji yote ya utalii Tanzania.

## Vivutio vya utalii

- **Sokwemtu;** Sokwe hawa wamefanya eneo hili kuwa paradiso nzuri na ni mahali ambapo mtu anaweza kufurahia kumwona kiumbe ambaye ni ndugu yake wa karibu pasipo adha ya kupanda milima kama ilivyo maeneo mengine ambayo yana milima.
- **Ziwa Victoria;** Ziwa hili linaongeza uzuri wa kisiwa hiki kwani ndilo ziwa kubwa kuliko yote barani Afrika na ziwa kubwa la kitropiki duniani.
- **Wanyama adimu kama Nzohe;** mnyama huyu adimu hupatikana kwa wingi katika kisiwa hiki.
- **Ndege;** Karibu spishi 400 za ndege zimebainishwa wakiwemo Kasuku-Kijivu wa kiafrika, Korongo, Hondohondo, Kulastara, na ndege wa mawindo wakiwemo Tai waishio kwenye maji.



- **Uoto wa asili;** Mchanganyiko wa makazi kutoka kwenye miti yenye uwazi mpaka vinamasi vya mianzi na misitu ya kijani kibichi hifanya hifadhi kuwa ya kuvutia sana
- **Meneo ya tamaduni;** Eneo la Ntungamirwe", "Maji Matakatifu", "Altare" na "Solo" ni maeneo yenye historia za kitamaduni kwa wakazi wanaoishi maeneo haya.
- **Irumo;** Eneo lenye kina kirefu kabisa cha ziwa Victoria
- **Fukwe;** Hifadhi hii ina fukwe nzuri za mchangani na michikoko.



## Shughuli za Kitalii

- Kutazama Sokwemtu. Utalii huu hufanyika kwa kupata uzoefu wa makazi ya sokwe. Chini ya usimamizi wa mwongoza utalii inawezekana kuwaendea sokwe kwa miguu na katika hali ya ukimya na kuwaangalia kwa kipindi kifupi;
- Kuendesha boti. Utalii huu hufanyika kwenye fukwe zenye miamba na kufanya aina hii ya utalii uwe wa kipekee na wa kufurahisha;
- Utalii wa kutwa kwa kutumia magari. Utalii huu hutoa fursa kwa wageni kuweza kuangalia wanyama wa aina mbalimbali kama Nzohe, Tembo, Viboko, Mamba na Twiga;
- Utalii wa kuvua samaki. Uvuvi huu unafanyika kwa kutumia boti ndogo ya michezo ya uvuvi katika maji yenye kina kirefu;
- Matembezi ya miguu. Utalii huu hufanyika kwa kutembea kwenye njia ndani ya msitu wa asili na ufukwe wa ziwa Victoria; na
- Utalii wa kutumia mtumbwi. Utalii huu hufanyika kwa mgeni kutumia mtumbwi kwa kutembelea eneo la maji la hifadhi na kujionea wanyama kama vile Viboko, Mamba na ndege wa aina mbalimbali.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema ya muda, hosteli na nyumba za kulala wageni zinazomilikiwa na hifadhi.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 736 778 493
Barua pepe: sitatunga@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 735 944 445
Instagram: rubondoisland_tz

# HIFADHI YA TAIFA
# KITULO



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Kitulo ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2005 ikiwa na eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 465. Hifadhi hii hujulikana kama *"Bustani ya Mungu"* kutokana na uwepo wa aina nyingi za maua kwenye uwanda uliotanda takribani mita 2,600 (8,500 ft) kwenye miinuko ya vilele vya Milima ya Kipengere, Poroto na Livingstone ambapo maua haya huchanua kati ya mwezi Desemba na Aprili.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Kitulo ipo Kusini mwa Tanzania katika mikoa ya Mbeya na Njombe kwenye wilaya za Makete, Rungwe na Mbeya vijijini.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za masika huanza kunyesha kuanzia mwezi Machi hadi Juni na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba. na ni kipindi kizuri cha kuona wanyama. Hifadhi hii inaweza kutembelewa nyakati zote za mwaka.



## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa Barabara;** Kutoka jiji la Mbeya-Isyonje-Kitulo ni kilomita 67; Jiji la Mbeya-Chimala-Kitulo ni kilomita 103: Kutoka Njombe mjini-Ikonda-Makete-Kitulo ni kilomita 165.

**Kwa njia ya Reli;** Kupitia usafiri wa reli kwa kutumia Reli ya Tanzania-Zambia (TAZARA) na kushuka katika stesheni za Makambako au Iyunga.

**Kwa anga;** Kupitia Uwanja wa Ndege wa KimaTaifa wa Songwe kisha kutumia barabara ambayo ni kilomita 83 kupitia makutano ya Isyonje kwenye barabara ya Uyole-Kyela na kilomita 125 kupitia makutano ya Chimala kwenye barabara ya Mbeya-Makambako.



## Vivutio vya utalii

- **Uwepo wa aina nyingi za maua;** Kuna zaidi ya aina 350 za mimea, zikiwemo aina 45 za mimea inayoota juu ya miti au katika matawi ya miti.
- **Wanyamapori;** Hifadhi ina Ndege, Pundamilia na baadhi ya swala wadogo wadogo. Eneo hili ni paradiso ya wapenzi wa ndege kwa sababu licha ya ndege wa kawaida kuna aina za ndege adimu kama vile Tandawala.
- Maporomoko ya maji
- Uoto na mandhari nzuri zenye milima na mabonde
- **Kilele cha mlima Mtorwi;** Kilele hiki kipo upande wa Mashariki mwa hifadhi na kina mwinuko wa mita 2,961 kutoka usawa wa bahari.
- **Ziwa la kasoko la Dhambwe;** Hili ni ziwa dogo la kasoko lililopo katikati ya hifadhi. Kwenye ziwa hili hupatikana ndegemaji wa aina mbalimbali.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutembea kwa miguu katika mbuga na kufuruahia maua hasa kuanzia mwezi Desemba hadi Aprili;
- Kutembelea maporomoko mbalimbali ya maji ndani ya Hifadhi ikiwemo yale yenye urefu wa mita 100 (Nhumbe);
- Matembezi ya muda mrefu ambapo mtalii ataweza kuona mandhari nzuri ya Ziwa Nyasa pamoja na ufukwe wake mzuri wa Matema; na
- Utalii wa kupanda milima

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni zinazomilikiwa na hifadhi. Kambi moja ya Umma ya kupiga mahema inapatikana ambayo ni Mwakipembo.

**Nje ya hifadhi;** Nyumba za kulala wageni zinapatikana katika mji mdogo wa Matamba, Chimala, jiji la Mbeya na Mji wa Njombe.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 734 041 852
Barua pepe: kitulo@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 767 536 130
Instagram: kitulo_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# MIKUMI



## Historia ya Hifadhi

Mikumi ilitangwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 1964 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 3,230. Eneo hili kubwa linaungana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (awali ikijulikana kama Selous) kwa kipande cha milima ya tao la mashariki kilichosheheni misitu, mito na ardhi oevu yenye miti mingi ya aina ya Miombo. Hifadhi hii ina sifa za kipekee ikiwa ni pamoja na uwepo wa makundi makubwa ya Nyati, kufikika kirahisi na kuona wanyama wengi kwa wakati mfupi.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Mikumi ipo Mashariki mwa Tanzania, katika mkoa wa Morogoro kwenye wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili kiangazi ni kuanzia mwezi Juni hadi Oktoba na Januari hadi Februari kwa mwaka ambapo mvua za vuli huanza kipindi cha mwezi Novemba hadi Desemba na mvua za masika huanza mwezi Machi hadi Mei. Hifadhi ya Taifa Mikumi inaweza kutembelewa nyakati zote za mwaka.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kirahisi kwa barabara ya kutoka Dar es salaam – Mbeya kilomita 283. Pia kutoka mji wa Morogoro kilomita 107.

**Kwa anga;** Hifadhi pia inafikika kwa njia ya anga kwa kutua kwenye uwanja uliopo ndani ya hifadhi wa Kikoboga.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Mikumi ina wanyama wakubwa wakiwemo Simba, Chui, Fisi, Mamba, Nyati, Tembo, Viboko, Twiga, Pundamilia, Pofu na spishi nyingine za wanyama wadogo wadogo.
- **Bwawa la viboko;** Bwawa hili ni eneo maarufu kwa uwepo kwa viboko na mamba hivyo kutoa fursa kwa wageni wanaokuja kutembelea hifadhi.
- **Tambarare ya Mkata na milima ya tao la mashariki;** Mandhari nzuri ya bonde la Mkata na safu za milima ya Rubeho zinaifanya hifadhi kuwa na mwonekano wa kuvutia sana.
- **Mawio na machweo ya jua;** Hifadhi ina maeneo mazuri kwa ajili ya kuangalia mawio na machweo ya jua ambapo wageni wanaweza kupata picha nzuri na za kupendeza.
- **Uoto wa asili;** Mchanganyiko wa aina mbalimbali za uoto wa asili hasa miombo na nyika zilizotawanyika imepelekea hifadhi hii kuwa na mvuto wa kipeke kabisa.





- **Ndege;** Hifadhi ina ndege zaidi ya jamii 400 wakiwemo wale wahamao na wasiohama.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kuangalia wanyama kwa kutumia gari;
- Utalii wa usiku wa kuangalia wanyama kwa kutumia gari;
- Utalii wa kutembea kwa miguu;
- Utalii wa kula chakula porini; na
- Utalii wa kupiga picha za filamu.


## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema na nyumba za wageni zinazomilikiwa na hifadhi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji mdogo wa Mikumi.

**Mawasiliano:**
Simu: +255 733 670 879
Barua pepe: mikumi@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 733 670 879
Instagram: mikumi_nationalpark

# HIFADHI YA TAIFA
# MILIMA YA MAHALE





## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale ilianzishwa mwaka 1985 ikiwa na eneo la kilomita za mraba 1,613 (kilomita za mraba 1,577 ikiwa ni eneo la nchi kavu na kilomita za mraba 96 zikiwa eneo la maji). Kuanzishwa kwa hifadhi hii ni matokeo ya jitihada za serikali ya kuamua kutunza Sokwemtu wachache waliokuwa wamebakia Afrika. Pia utunzaji wa eneo hili ni matokeo ya tafiti zilizofanywa na watafiti toka Japani kuanzia miaka ya 1965 ambapo walianza kwa kuwazoesha Sokwemtu kuwazoea binadamu kuanzia miaka ya 1966. Kwa wale wanaopendelea sehemu zilizojitenga, mandhari na mbuga nzuri, Hifadhi ya Taifa, Milima Mahale, kwa hakika, ndio chaguo nzuri la sehemu ya kutembelea hapa Afrika

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale ipo Magharibi mwa Tanzania, katika mkoa wa Kigoma kwenye wilaya ya Uvinza.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi hadi Desemba na mvua za masika huanza mwezi Machi hadi Mei. Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale inaweza kutembelewa nyakati zote za mwaka, kipindi cha kiangazi ni kuanzia mwezi Juni hadi Oktoba na ni wakati mzuri wa kuona wanyama.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Kutoka Kigoma hifadhi inafikika kwa njia barabara yenye umbali wa kilometa 220 kutoka mji wa Kigoma.


**Kwa maji;** Hifadhi inaweza kufikika kwa boti za binafsi zinazoweza kukodiwa kutoka Kigoma kwa ajili ya safari. Wageni wanaweza pia kutumia boti za abiria zinazoenda kusini mwa Kigoma kupitia Hifadhini.

**Kwa anga;** Njia rahisi kabisa ya kwenda na kurudi kutoka Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale ni kwa njia ya ndege kwa kutumia uwanja mdogo uliopo hifadhini. Ndege za kukodi kutoka Dar es salaam, Zanzibar, Arusha na majiji/miji mikubwa zinapatikana kwa urahisi.

## Vivutio vya utalii

- **Sokwemtu;** Sokwe hawa huonekana kwa urahisi ndani ya msitu na wakati mwingine utawakuta wakitembea chini ya ardhi. Ni wanyama wanaoishi kijamii na huwa na taratibu zao za uongozi. Sokwe hawa ni kivutio kikubwa kwa watalii wanaokuja kutembelea hifadhi hii.
- **Ziwa Tanganyika;** Ziwa Tanganyika ndiyo ziwa refu kuliko maziwa yote Barani Afrika lenye urefu wa kilomita 673 na kina cha urefu wa kilomita moja na nusu na lina takribani asilimia 16 ya maji baridi yote





ulimwenguni. Ni la pili kwa ukubwa duniani na ndilo ziwa lenye maji safi duniani. Ziwa hili ni makazi ya mamia ya aina za samaki na wanyama kama Viboko na Mamba.

- **Safu za Mlima Mahale;** Mlima huu unatoa fursa ya kipekee kwa watalii wanaopenda kupima uwezo wa miili yao kwa kukwea hadi kileleni.
- **Mchanganyiko wa Wanyama na Mimea;** Mchanganyiko wa mimea ya ukanda wa Magharibi na Kusini kunaifanya hifadhi hii iwe na msitu mnene ambao umesheheni wanyama wa aina mbalimbali ikiwepo aina tisa za wanyama jamiii ya primata.
- **Mwonekano mzuri wa mazingira;** Mchanganyiko wa misitu, safu za milima na ziwa kunaipa hifadhi mwonekano mzuri na wenye kuvutia.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- **Kutizama Sokwemtu.** Utalii huu hufanyika kwa kuwafuata Sokwe na kujionea jinsi wanavyoishi wakiwa porini;
- **Matembezi ya siku kwenye njia za asili.** Hifadhi pia inatoa fursa nzuri ya matembezi kwenye njia za asili zilizobuniwa kwa ustadi mkubwa na wakati wa matembezi utaweza kuona wanyama wengine kama Viboko, Mamba, Swala, Simba na Chui;
- **Kuendesha boti ziwani.** Utalii huu unamwezesha mtalii kuona mandhari nzuri ya ziwa na kuwa karibu na maji huku akizungukwa na fukwe nzuri zilizojaa ndegemaji, Mamba, Viboko na mimea mbalimbali.
- **Utalii wa kuvua samaki.** Utalii huu hufanyika ziwani ambapo samaki akishavuliwa huwa anarejeshwa kwenye maji ili waendelee na maisha yao ya kawaida;
- **Kupanda Mlima Mahale.** Utalii huu hufanyika kwa kupanda hadi kilele cha Kungwe chenye urefu wa mita 2,462 kutoka usawa wa bahari; na
- **Kupiga Makasia.** Utalii huu hufanyika kwa kutumia mitumbwi midogo ambapo watalii wanapata fursa ya kuwa karibu zaidi na mazingira ya kwenye maji na pia kuangalia ndege wa aina mbalimbali.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi:** Kuna maeneo ya kupiga mahema ya muda, kambi za mahema za kudumu na nyumba za kulala wageni zinazomilikiwa na hifadhi.

**Nje ya hifadhi:** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji wa Kigoma.


**Mawasiliano:**

Simu: +255 282 988 244
Barua pepe: mahalemountains_nationalpark
Instagram: mahalemountains_nationalpark

# HIFADHI YA TAIFA
# MILIMA UDZUNGWA



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa ilianzishwa mwaka 1992 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1,990. Hifadhi hii imehifahdi eneo kubwa la milima ya tao ya Mashariki na ina spishi mpya kabisa ya kima aitwaye Kipunji mwenye kope nyeupe anayepatikana Tanzania tu na yupo hatarini kutoweka ambae aligundulika mwaka 1979. Pia kuna spishi mpya ya Kware ambaye kwa mara ya kwanza iligunduliwa na wanasayansi mwaka 1992 na kumwita Kware wa Misitu ya Udzungwa.



## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa ipo Mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Iringa na Morogoro kwenye wilaya za Kilombero na Kilolo.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za vuli ni kuanzia mwezi Novemba hadi Desemba na kipindi cha masika ni kuanzia mwezi Machi hadi Mei. Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa inaweza kutembelewa nyakati zote za mwaka, kipindi cha kiangazi kinaanzia mwezi Juni hadi Oktoba na ni kipindi kizuri cha kuona wanayama na kupanda mlima.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, anga na treni.

**Kwa barabara;** Kutoka Dar es Salaam, kwa kutumia barabara ya Morogoro kupitia Chalinze, Morogoro mjini, Hifadhi ya Taifa Mikumi mpaka Mikumi mjini. Kutoka Mikumi mjini, tumia njia ya kushoto ukifuata



vibao vya Ifakara na barabara hii itakufikisha hadi Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa.

**Kwa treni;** Treni kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia hupita karibu na hifadhi ambapo kuna stesheni ya treni ya Mang'ula karibu kabisa na makao Makuu ya hifadhi.

**Kwa anga;** Kuna viwanja viwili kwa ajili ya ndege ndogo vya Msolwa na Kilombero vinavyoweza kutumika na watalii kwa usafiri wa anga na kumalizia safari zao kwa usafiri wa gari/barabara kuja katika lango la kuingia hifadhini. Pia unaweza kutua kwenye uwanja wa Ndege wa Hifadhi ya Taifa Mikumi kisha kutumia barabara kuelekea hifadhini.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi ina aina nyingi za wanyama. Pia ni eneo ambalo wanapatikana kima wa kipekee aitwae Kipunji ambae hapatikani eneo lingine popote duniani.
- **Uoto wa asili;** Hifadhi imepambwa na msitu mnene uliopo kwenye tao la milima ya Mashariki.
- **Maporomoko ya maji;** Mwonekano mzuri wa msitu unapambwa na maporomoko makubwa ya maji ya Sanje.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Kupanda milima. Udzungwa ina mtandao wa njia za watembea kwa miguu uliosanifiwa vizuri kwa ajili ya kupanda milima iliyopo. Zipo njia za matembezi ya saa moja (Sonjo hike) mpaka zile za muda mrefu wa



masaa sita kupitia njia ya Rumemo;
- Matembezi kwenye njia za asili;
- Kuangalia wanyama adimu;
- Kuangalia ndege;
- Utalii wa michezo;
- Utalii wa mikutano; na
- Kumzoesha na kumfuatilia kima aina ya Kipunji

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema ya jumuiya na binafsi na pia yapo malazi kwenye koteji zinazomilikiwa na hifadhi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji mdogo wa Mangula.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 738 070 257
Barua pepe: udzungwa@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 717 468 751
Instagram: udzungwamountain_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# MKOMAZI



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Mkomazi ilipandishwa hadhi kutoka Pori la akiba na kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2008 ikiwa na eneo la kilomita za mraba 3,245. Asili ya jina Mkomazi ni maneno mawili kutoka katika kabila la Wapare ambalo ni kundi la jamii inayozungumza lugha ya kibantu nchini na wanapatikana katika Mkoa wa Kilimanjaro. "Mko" maana yake kijiko cha asili cha Wapare na "Mazi" ni maji. Inaaminika maneno haya yana tafsiri ya uhaba wa maji katika eneo hili hasa wakati wa kiangazi. Ni eneo unaloweza kufurahia wanyamapori, vichaka vyenye miiba, mibuyu, vilima na pia unaweza kuona Mlima Kilimanjaro kwa karibu kutoka maeneo yote ya Hifadhi.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Mkomazi ipo Kaskazini Mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Kilimanjaro na Tanga kwenye wilaya za Mwanga, Same, Lushoto, Korogwe na Mkinga.

## Hali ya hewa

Hifadhi hii ina misimu miwili kwa mwaka ambapo mvua za muda mfupi hunyesha mwezi Novemba hadi Desemba na mvua za muda mrefu hunyesha mwezi Machi hadi Mei. Mwezi Juni hadi Septemba na Januari hadi Februari ni msimu wa kiangazi ambapo hali ya hewa ni ya ukavu na joto.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi ya Mkomazi inafikika kwa barabara na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kwa barabara kutokea jiji la Arusha kilomita 202, kilomita 140 kutoka Uwanja wa KimaTaifa wa Kilimanjaro (KIA), kilomita 110 kutoka mji wa Moshi na kilometa 550 kutoka Jiji la Dar-es Salaam.

**Kwa anga;** Hifadhi inafikika kwa ndege za kukodi kutoka sehemu mbalimbali za nchi na kutua kwenye viwanja vya ndege vya Kisima na Mkomazi vilivyopo ndani ya hifadhi.

## Vivutio vya utalii

- **Faru na Mbwamwitu;** Hifadhi ya Taifa Mkomazi ina Faru na Mbwamwitu ambao ni adimu sana duniani. Ni fursa ya kipekee kwa watalii wanaotembelea hifadhi kuona wanyama hawa ambao huonekana mara chache katika hifadhi nyingine nchini.
- **Swala Adimu;** Hifadhi ina swala adimu kama vile Swalatwiga, Choroa na Tandala wadogo wanaoonekana kwa makundi katika maeneo ya mbuga na vichaka. Swala hawa ni sababu tosha inayomfanya mtalii asiweze kukosa kutembelea hifadhi hii.
- **Wanyama wakubwa na wadogo;** Wanyama wanaopatikana kwenye hifadhi hii ni aina ya wanyama wapatikanao kwenye maeneo ya nusu jangwa. Wanyama kama, Tembo, Nyati, Twiga, Nyumbu,



Kudu, Swala, na wanyama wawindao kama Simba, Chui na Duma wote kwa pamoja huishi kwenye mazingira ya hifadhi hii jambo ambalo linaifanya kuwa na mvuto wa kipekee.

- **Ndege;** Hifadhi hii ina aina zaidi ya 450 za ndege ambazo huonekana kirahisi wakati wa kufanya utalii wa kutumia gari au kutembea kwa miguu. Aina za ndege ambao huonekana kwa urahisi ni pamoja na Shorobo Buluu, Mbuni, Tai Ushungi, Tandawala, Njiwa na Tetere, Hondohondo, Kanga na Kware.
- **Uoto wa asili;** Mkomazi inafanya ukanda wa mwisho wa uoto wa asili wa 'Sahel' kwa upande wa Kusini ambapo uoto huu unaifanya hifadhi iwe na mwonekano wa kijangwa. Kutokana na hali hii, uoto wa asili umetawaliwa na mikunga hasa aina ya Mkunga Filimbi. Kwa upande wa Magharibi ambapo kuna milima, uoto wa asili hubadilika na kuwa misitu ya ardhi kavu.
- **Mandhari nzuri;** Hifadhi ina mandhari nzuri ya uoto kwa asili ambao haupatikani sehemu nyingine yeyote kwenye Hifadhi zingine za Taifa Tanzania na unapata fursa ya kuwa katikati ya mandhari nzuri ya milima ya Pare, Usambara na Kilimanjaro.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kutumia gari. Utalii wa kutumia gari ni maarufu kwa hifadhi ya Mkomazi na hutoa fursa kubwa kwa mtalii  kuweza kuona vivutio mbalimbali;
- Utalii wa kutembea kwa miguu. Utalii huu ambao hufanyika pamoja na askari muongoza watalii ni aina ya utalii ambao hutoa fursa kwa watalii kuona vivutio vingi na kwa karibu zaidi;
- Kupanda milima. Utalii huu hufanyika kwa kupanda vilele vya milima inayopatikana hifadhini na vilele vya milima ya Tao la Mashariki;
- Utalii wa kutazama Ndege. Hifadhi ya Taifa Mkomazi ni makazi ya aina za ndege zaidi ya 450 ambao wana makazi ya kudumu na wengine ni wahamaji kutoka Ulaya, Asia ya Kaskazini na maeneo mengine ya bara la Afrika. Mtalii anaweza kuona aina za ndege zaidi ya 100 kwa siku moja;
- Utalii wa kupiga picha na filamu. Huu ni utalii unaofanywa na watalii wanaopenda kupiga picha na kuchukua filamu za wanyamapori kwa kutumia kamera na vifaa maalum. Hifadhi ya Mkomazi ni sahihi kabisa kwa utalii huu kwa kuwa ina vivutio vingi ikiwa ni pamoja na wanyama adimu kama Mbwamwitu na Faru mweusi.
- Utalii wa usiku wa kutumia gari. Utalii huu hufanyika kwa kutumia gari nyakati za usiku ukiwa na askari. Watalii hupata fursa ya kuona wanyama wanaopenda kufanya shughuli zao nyakati za usiku hasa wanyama jamii ya paka.
- Utalii wa Faru. Huu ni utalii wa kipekee unaovutia wageni wengi kutembelea hifadhi hii. Utalii huu unafanywa kwa kutumia magari ya hifadhi  na askari kiongozi. Mtalii atapata fursa  kujifunza maisha ya faru, historia yao na  kuona Faru kwa ukaribu zaidi.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Hifadhi ina aina mbalimbali za malazi ikiwa ni pamoja na kambi za jumuiya, kambi maalum na nyumba za kulala wageni (Koteji). Pia kuna kambi za kudumu na kambi ya muda mfupi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna Hoteli, Loji na  nyumba za kulala wageni katika mji wa Same.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 27 297 4165
Barua pepe: mkomazi@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 624 333 888
Instagram: mkomazi_park_tanzania

# HIFADHI YA TAIFA
# MTO UGALLA



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla ilipandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2019, ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 3,865. Hifadhi hii imepitiwa na Mto Ugalla ambao ni mto wa pili kwa urefu Tanzania. Mto huu hutiririsha maji yake taratibu kuelekea Magharibi na kuvuka mipaka ya Hifadhi kuelekea kwenye eneo la ardhi oevu lenye Vinamasi vya Moyowosi ambapo mwishowe hutiririka kuelekea Ziwa Tanganyika.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla ipo Magharibi mwa Tanzania katika mkoa wa Tabora kwenye wilaya za Kaliua, Urambo na Mpanda.

## Hali ya hewa

Hali ya hewa ya hifadhi ni ya kitropiki ambapo msimu wa mvua ni kuanzia mwezi Novemba hadi Mei na kipindi cha Kiangazi ni kuanzia mwezi Juni hadi Novemba na ndio muda mzurii kwa Utalii. Wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya Milimita 800 hadi 1000 wakati hali ya joto kwa nyakati za kiangazi ni kati ya nyuzijoto za sentigredi 28 hadi 30 na kwa kipindi cha mvua ni kati ya nyuzijoto za sentigredi 15 hadi 21.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, anga na treni.

**Kwa barabara;** Kwa kipindi cha kiangazi kuanzia mwezi Juni hadi Novemba, hifadhi inafikika kwa njia ya barabara kutoka mji wa Tabora ni kilomita 170, kutoka Wilaya ya Kaliua ni kilomita 45 na kutoka Wilaya ya Urambo ni kilomita 75.

**Kwa treni;** Hifadhi inafikika kupitia reli ya Tabora – Kigoma na kushuka kituo cha Usoke na Kaliua. Pia reli ya Mpanda – Kaliua na kushuka kituo cha Lumbe au Ugalla.

**Kwa anga;** Kwa kutumia ndege za kukodi, hifadhi inafikika kupitia viwanja vya ndege vilivyo karibu vya Tabora, Urambo na Kaliua. Pia wageni wanaweza kutumia viwanja vya ndege vilivyopo hifadhini vya Muhuba, Siri na Kasense ambapo viwanja hivi vinatumika kipindi cha kiangazi tu.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi hii ina aina nyingi za wanyama kama vile Tembo, Simba, Chui, Mbwamwitu, Fisi, Mbweha, Nyamera, Korongo, Palahala, Tandala, Kongoni, Nyati, Funo, Pofu, Oribi, Tohe, Pundamilia, Mamba na Nzohe ambao wanapatikana zaidi maeneo oevu ya Magharibi mwa hifadhi.





- **Uoto wa asili;** Hifadhi imepambwa na aina mbili za uoto wa asili ambapo uoto wa kwanza ni ule wa miombo na wa pili ni uoto wa Zambezi wenye maeneo ya nyasi zenye maji mengi. Aina hii ya uoto unaifanya hifadhi kuwa ya kipekee kwa wageni kutalii.
- **Mandhari mazuri;** Mwonekano mzuri wa mikunjo ya mito, mabonde na nyika kubwa zilizopambwa na vilima vinaipa hifadhi mwonekano wa kipekee na unaovutia
- **Vichuguu vya mchwa;** Uwepo wa vichuguu vya mchwa vinavyojitokeza kwenye ardhi ya tambarare vinatoa mazingira mazuri kwa wanyama wawindao ambapo husimama juu yake na kuangalia mawindo yao.
- **Mto Ugalla;** Mto huu unaopita katikati ya hifadhi ndio kivutio kikuu ambapo unatoa mazingira mazuri kwa wanyama wa aina mbalimbali. Pia mto unatoa fursa nzuri kwa watalii kuona wanyama kwa urahisi. Mto huu ndio uhai wa hifadhi hii kwani unatoa makazi kwa wanyama wa ardhini na wale wanaoishi kwenye maji na ndio chanzo kikuu cha maji kwa kipindi cha kiangazi.
- **Mamba wakubwa;** Hifadhi hii ina mamba wakubwa kabisa ambapo katika historia ndio eneo pekee lenye mamba wakubwa Afrika. Kwa kipindi cha mvua mamba hawa wanakula zaidi samaki na kwa kipindi cha kiangazi huwa wanawinda wanyama ili kujitosheleza kwa chakula.
- **Maeneo ya Kihistoria;** Kuwepo kwa maeneo ya kihistoria ya Mfinula iliyopo Ikunkwa, Senga II na Ilyamchele kunatunza historia na tamaduni ya wakazi walioshi maeneo haya.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Matembezi ya kutwa kwa kutumia gari. Kwa kutumia njia za utalii na hasa kufuata Mto Ugalla ambao una mandhari mazuri ya maziwa, mikunjo na ukiwa umepambwa na wanyama wa aina mbalimbali;
- Matembezi ya miguu. Utalii huu hufanyika nyakati za asubuhi na jioni ambapo ni wakati mzuri wa wanyama kuonekana kwa urahisi kwani joto linakuwa chini na pia ni wakati ambao wanyama wanakuwa wanajitafutia chakula. Aina hii ya utalii inakuweka karibu zaidi na mazingira ya asili huku ukifurahia sauti za wanyama, ndege na wadudu wa msituni; na
- Kutazama ndege. Hifadhi inatoa nafasi nzuri kwa watalii wanaopenda kutazama ndege kwani eneo hili lina aina 147 za ndege ikijumuisha ndege wakazi na wale wahamao.

## Huduma za malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema ya jumuiya na binafsi.

**Nje ya hifadhi:** Kuna nyumba za kulala wageni kwenye mji mdogo wa Kaliua.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 739 302 443 / +255 754 469 865
Barua pepe: ugallariver@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 784 302 443
Instagram: ugalla_river_nationalpark

# HIFADHI YA TAIFA NYERERE



© Robert J. Ross

## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Nyerere ni hifadhi kubwa kuliko zote Tanzania. Ilianzishwa mwaka 2019 na ina eneo la kilomita za mraba 30,893. Hii inaifanya kuwa Hifadhi ya Taifa ya tatu kwa ukubwa barani Afrika baada ya Namib-Nankluft iliyopo nchini Nambia na hifadhi ya Taifa Salonga iliyopo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Hifadhi hii imetokana na kumegwa sehemu ya Pori la akiba Selous na kutangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa. Ilipewa jina "Nyerere" kwa heshima ya Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Julius Kambarage Nyerere ambaye mwenyewe alikuwa na uhifadhi wa dhati.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Nyerere inapatikana Kusini Mashariki mwa Tanzania katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi na Ruvuma; kwenye wilaya za Rufiji, Kisarawe, Morogoro, Kilombero, Ulanga, Namtumbo, Liwale, Tunduru , Kilosa na Malinyi. Inapakana na Hifadhi ya Taifa Mikumi kwa upande wa Kaskazini Magharibi na Pori la akiba Selous upande wa Kusini Mashariki.

## Hali ya hewa

Hali ya hewa katika Hifadhi ya Taifa Nyerere ni ya misimu miwili ya mvua. Mvua za masika hunyesha kuanzia mwezi Machi hadi Mei na mvua za vuli hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Desemba. Mwezi Juni hadi Septemba na Januari hadi Februari ni msimu wa kiangazi

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, treni na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kwa gari kutoka jijini Dar es Salaam kupitia Kibiti hadi lango la Mtemere umbali wa Kilomita 240. Pia kutoka mji wa Morogoro kupitia Kisaki hadi lango la Matambwe, kilomita 161 ambapo ndipo yalipo Makao Makuu ya Hifadhi.

**Kwa treni;** Hifadhi inafikika kwa njia ya reli ya TAZARA inayopita hifadhini na baadhi ya vituo vya treni ni Fuga na Matambwe.

**Kwa anga;** Hifadhi inafikika kwa ndege za kukodi kutoka sehemu mbalimbali za nchi na kutua kwenye viwanja vya ndege vilivyopo hifadhini.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi hii ina wanyamapori wengi, wakubwa na wadogo kama vile Simba, Chui, Fisi Mbwamwitu, Tembo, Nyati, Viboko, Pundamilia, Nyumbu, Korongo, Tandala wakubwa na wadogo na Mamba. Aidha kuna ndege wa aina mbalimbali wa nchi kavu na ndegemaji kama vile Mbuni, Batamaji, Tai, Tandawala na wengine wengi.
- **Mto Rufiji;** Mto huu ndio mkubwa kuliko mito yote Tanzania. Mto huu unapita hifadhini kutokea upande wa Kaskazini na unatiririsha maji yake polepole na kutengeneza vinamasi kadhaa vinavyochangia uzuri wa mandhari ya Hifadhi. Mto huu ambao humwaga maji yake kwenye bahari ya Hindi, unafahamika




kuwa na idadi kubwa ya wanyama jamii ya Viboko na Mamba.

- **Idadi kubwa ya Tembo na Mbwamwitu;** Hifadhi inasifika kwa kuwa na idadi kubwa ya Tembo na Mbwamwitu barani Afrika ambapo Mbwamwitu hawa ni wanyama adimu na waliopo hatarini kutoweka.
- **Aina mbalimbali za ndege;** Hifadhi ya Taifa Nyerere ina aina 440 za ndege ambazo zimeaninishwa. Wengi wao ni ndege wakaazi wa eneo hili na wachache wahamao kutoka nchi za Ulaya, Asia ya Kaskazini na maeneo mengine ya Afrika. Ndege hao wanapatikana katika maeneo ya mito, misitu, ukanda wa nyasi na mbuga. Katika idadi hii ya ndege walioanishwa kuna ndege adimu kama vile jamii ya bundi wavuao samaki (Pel's Fishing Owl) na Korongo Mgongomweupe.
- **Aina adimu ya Jamii za Swala;** Kutokana na uoto wa asili wa Miombo uliopo katika Hifadhi ya Taifa Nyerere, jamii adimu za wanyama kama vile Korongo, Palahala, Kongoni jamii ya "Lichtenstein" na Nyumbu jamii ya Nyasa wanapatikana.
- **Bwawa la Umeme la Nyerere;** Katika Hifadhi ya Taifa Nyerere kuna bwawa maarufu linalojulikana kama ''Bwawa la Nyerere''. Bwawa hili pamoja na uzalishaji wa umeme pia ni kivutio kikubwa cha utalii kutokana na ukubwa wake na teknolojia iliyotumika bila kuathiri mazingira ya Hifadhi.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa kwa kutumia magari. Utalii wa kutumia magari ni maarufu katika hifadhi kwani humpatia mtalii fursa ya kuona wanyama mbalimbali kwa kupita kwenye barabara zilizotengenezwa mahususi kwa ajili ya utalii huo;
- Utalii wa kutembea kwa miguu. Utalii huu ambao hufanyika pamoja na askari muongoza watalii ni aina ya utalii ambao hutoa fursa kwa watalii kuona vivutio kwa karibu zaidi pengine kuliko aina nyingine za utalii;
- Utalii wa boti. Kutokana na kuwepo kwa mto Rufiji pamoja na maziwa, watalii wanapata fursa ya kufurahia utalii wa boti. Utalii huu huwafikisha watalii sehemu ambazo haziwezekani kufikika kwa magari au miguu;
- Utalii wa kula chakula porini, Utalii huu ni wa kipekee kwani humpatia fursa mtalii kula chakula cha moto akiwa porini huku akiwa anatazana wanyama na mandhari nzuri ya hifadhi; na
- Utalii wa kupiga picha. Utalii huu unafanyika hifadhini na watalii wanaopenda kupiga na kutengeneza filamu za wanyamapori kwa kutumia magari maalum au boti.

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Hifadhi ina aina mbalimbali za malazi ikiwa ni pamoja na kambi za jumuia, kambi maalum, kambi za msimu na kambi za kudumu. Pia zipo loji na kambi zinazomilikiwa na watu binafsi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika miji ya Iringa, Morogoro, Kisaki na Mikumi.

### Mawasiliano

| | |
|---|---|
| Simu: | +255 232 935 351 / +255 232 935 352 |
| Barua pepe: | ugalla@tanzaniaparks.go.tz |
| Whatsapp: | +255 762 012 700 |
| Instagram: | nyerere_national_park |

# HIFADHI YA TAIFA
# RUAHA



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Ruaha ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 1964 na kisha ikaongezewa eneo la bonde la Ihefu mwaka 2008 na kufikia ukubwa wa kilomita za mraba 20,226 na kuifanya kuwa Hifadhi ya pili kwa ukubwa hapa Tanzania. Hii ni takribani sawa na ukubwa wa jimbo la New Jesey ya nchini Marekani, au sawa na ukubwa wa nchi ya Wales ya huko Ulaya. Kimsingi Ruaha, ni sehemu ya mfumo mkubwa wa ikolojia wenye takribani kilomita za mraba 45,000. Hifadhi hii inapambwa na uwepo wa mito, milima, nyanda za tambarare, miinuko, mibuyu, vilima, marundo ya masalia ya miamba ya kale, misitu minene, ardhi oevu na uoto wa savana uliosambaa, vyote hivi vinaifanya hifadhi hii iwe ya mvuto sana kwa wageni.

Hifadhi hii ndipo unapopita mto pekee, Mto Ruaha Mkuu ambao unatiririsha maji hadi Kaskazini Mashariki mwa hifadhi. Kwa kipindi cha kiangazi mto huu unapungua maji lakini ndio chanzo kikuu cha maji kwa wanyama na hii inatoa fursa kwa wageni kujionea wanyama wengi kwa nyakati hizi za kiangazi.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ipo Magharibi mwa Tanzania katika Mikoa ya Iringa na Mbeya kwenye wilaya za Iringa, Mbarali, Chunya, Chamwino na Mufindi.



## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za masika huanza kunyesha kuanzia mwezi Machi hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi ipo takribani kilomita 108 kutoka mji wa Iringa na kilomita 625 kutoka jiji la Dar es salaam.

**Kwa anga;** Zipo ndege za kawaida na za kukodi kwenda hifadhini kutokea miji/jiji la Arusha, Dodoma, Kigoma na Dar-es-salaam. Viwanja vidogo vya hifadhi viko Msembe na Jongomero.



## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Kuna makundi makubwa ya Tembo na Nyati ambao ni sehemu ya wanyama wakubwa (Big Five) na wanyama adimu kama vile Palahala, Korongo, Tandala Wakubwa na Wadogo na swala wadogo wadogo.
- **Maeneo ya kitamaduni;** Kuna maeneo ya kitamaduni kama vile nyumba ya Makumusho ya Mtwa Mkwawa na Isimila yenye vitu vya kale.
- **Idadi kubwa ya ndege;** Kimsingi kuna zaidi ya aina 574 za ndege zilizosajliwa.
- Pia hifadhi ina idadi kubwa ya wanyama wawindao hasa Mbwamwitu, Chui, Duma, Simba na Mamba.
- **Mto Ruaha mkuu;** Mto huu ni kivutio kikubwa kwa wageni kwani mbali na mandari yake ya kuvutia, ni maeneo ambao wanyama wa aina nyingi wanapatikana hasa nyakati za kiangazi.
- **Samaki aina ya Taiga;** Aina hii ya samaki ni adimu na hutoa fursa ya kufanya utalii wa michezo ya kuvua samaki na kuwarejesha tena kwenye maji
- **Uoto wa asili;** Hifadhi ina uoto wa kipekee wa asili wenye mwingiliano kati ya kanda ya Mashariki na Kusini.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kutumia gari;
- Utalii wa kutembea kwa miguu kwa kusindikizwa na mwongoza wageni mwenye silaha;



- Utalii wa usiku kwa kutumia magari katika maeneo yaliyoruhusiwa;
- Utalii wa kuvua samaki;
- Kuangalia ndege;
- Utalii wa puto (baluni)
- Utalii wa Boti

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna vituo vya kambi za umma, kambi binafsi, kambi za msimu, nyumba ya kupumzika wageni, malazi yanayotolewa na makampuni binafsi, hoteli na kambi za kudumu.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji wa Iringa.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 756 144 400
Barua pepe: ruaha@tanzaniaparks.go.tz
Instagram: ruaha_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# RUMANYIKA-KARAGWE





## Historia ya Hifadhi

Rumanyika-Karagwe ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2019 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 247. Hifadhi ina pori kubwa, mandhari nzuri na ina fursa nyingi kwa ajili ya utalii wa picha. Kitu muhimu katika eneo hili ni bonde refu lenye mto wenye mikunjo ambapo unagawanyika katika maziwa na vinamasi. Miteremko ya chini ya bonde inapendezeshwa na nyasi za savana na vipande vya misitu pamoja na vichaka vikubwa.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe ipo Magharibi mwa Tanzania katika mkoa wa Kagera kwenye wilaya za Karangwe, Ngara, Biharamulo na Kyerwa.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za masika huanza kunyesha mwezi Februari hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, maji na anga.

**Kwa barabara;** Kutoka Bukoba -wilayani Kyerwa-Rumanyika-Karagwe ni 180 km na kutoka Chato mpaka Murongo ni kilomita 327. Vilevile kwa kutumia barabara kupitia







Uganda na Rwanda,  Kikagati mpaka Murongo au kutoka Rwanda kupitia Rusumo, Karagwe mpaka Murongo.

**Kwa anga:** Kuna viwanja vya ndege vya Chato na Bukoba ambavyo ndege za kwaida zinaweza kuruka na kutua kwenye uwanja mdogo wa ndege wa Ibanda-Kyerwa.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Wapo wanyama wa aina mbalimbali kama vile Nyati, Nzohe, Kuro, Chui, Funo, Tumbili, Nyani, Tembo na aina nyingi za ndege.
- **Mawio na machweo ya jua;** Hifadhi ina mwonekano mzuri wa machweo na mawio ya jua ambapo kunatoa fursa kwa watalii kupata picha nzuri za mwonekano wa hifadhi.
- **Uwepo wa Mabwawa mengi:** Hifadhi ina mabwawa ambayo ni vyanzo vya maji na makazi ya wanyama mbalimbali.
- **Mandari nzuri;** Hifadhi ina mandhari mazuri ya mazingira yenye mito, mabonde, msitu mnene wa asili.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kuangalia wanyama kwa gari;
- Utalii wa kutembea kwa miguu;
- Kutazama ndege;
- Kuweka kambi;
- Kuendesha mitumbwi;
- Utalii wa kuvua samaki; na
- Utalii wa boti.

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema ya jumuiya na binafsi yanayomilikiwa na hifadhi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji wa Murongo.

**Mawasiliano:**

Barua pepe: ir@tanzaniaparks.go.tz
Instagram: rumanyikakaragwe_national_park

# HIFADHI YA TAIFA SAADANI



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Saadani ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2005 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1,100. Hifadhi hii ni ya kipekee Afrika Mashariki inayokutanisha eneo la nyika na bahari. Hifadhi ipo katikati ya miji ya kihistoria ya Bagamoyo, Pangani na Zanzibar.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa Saadani ipo Mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Pwani, Dar es Saalam na Tanga kwenye wilaya za Bagamoyo, Pangani na Handeni.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua, ambapo mvua za masika huanza kunyesha mwezi Machi hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu mrefu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba. Mwezi Januari hadi Februari ni miezi ya kiangazi kifupi.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara, maji, anga na reli.

**Kwa barabara;** Kutoka Dar es salaam, Bagamoyo – Makurunge kuingilia lango la Wami (Gama) ni kilomita 120. Kutokea Tanga – Pangani – Mkwaja kuingilia lango la Madete ni kilomita 130 na kutokea njia panda Chalinze – Mandera, Miono kuingilia lango la Mvave ni kilomita 110. Kutokea Dar es salaam kupitia Chalinze - Mandela,Miono na kuingilia lango la Mvave ni kilomita 220.

**Kwa maji;** Unaweza kufika Hifadhi ya Taifa Saadani kwa kutumia mtumbwi au boti za kukodi kutoka miji ya Zanzibar, Bagamoyo, Dar es Salaam na Tanga.

**Kwa anga;** Hifadhi inafikika kwa kutumia kiwanja kidogo cha ndege kilichopo hifadhini.

**Kwa reli:** Hifadhi pia inafikika kirahisi kwa njia ya reli ya Kaskazini ambayo huanzia Dar es salaam kupitia hifadhini, geti la Mvave ambapo ni kilomita 161.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Kuna aina mbalimbali za wanyama kama Twiga, Tembo, Kuro, Nyati, Simba, Viboko, Mamba, Nyani, Ngiri, Palahala na wengine wengi.
- **Delta ya mto Wami;** Delta hii ina msitu mnene wa mikoko na makundi ya Viboko, Mamba pamoja na aina mbalimbali za ndege.
- **Mazalia ya kasa wa kijani;** Mtalii/Mgeni anaweza kuwa na bahati ya kuona na kushuhudia muda halisi wa kuangua.
- **Mandhari;** ya kuvutia ya fukwe pamoja na muunganiko wa nyika na bahari.





- **Ndege;** Hifadhi hii ina aina mbalimbali za ndege wakiwepo wale wa kuhamahama.
- **Misitu minene;** Hifadhi ina msitu mnene ambao upo pwani ya Afrika Mashariki eneo la Zaraninge.
- **Mabaki ya kihistoria ya ukoloni;** Mabaki haya yanahusiana na biashara ya utumwa karne ya 19 pamoja na utamaduni, mila na desturi ya wenyeji wa pwani.
- **Aina mbalimbali za viumbe wa baharini;** Hifadhi hii ni ya kipekee kabisa ukilinganisha na hofadho nyingene za taifa kwani itaoa fursa kwa watalii kuweza kuona wanyama na viumbe mbalimbali waishio baharini.
- **Fungu la mchanga Mafui;** Mchanga huu hujitokeza nyakati za kubwa kwa bahjari na kufanya kisiwa kizuri cha mchanga ambapo watalii wanaweza kutalii na kufanya shughuli mbalimbali kama vile michezo ya baharini

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kuangalia wanyama kwa kutumia magari;
- Utalii wa kuangalia wanyama nyakati za usiku kwa kutumia magari;
- Utalii wa kutembea kwa miguu;
- Safari za boti Mto Wami;
- Utalii wa fukwe na mapumziko katika fukwe safi ya bahari ya Hindi;
- Kushuhudia wakati halisi Kasa wa kijani wanapoanguliwa;
- Kufanya safari za boti baharini na kutembelea fungu la mchanga la Mafui;
- Michezo mbalimbali ya ufukweni katika Bahari ya Hindi; na
- Kutembelea kijiji cha uvuvi cha Saadani, ambacho kimo ndani ya hifadhi, ambapo kuna maeneo mazuri ya mabaki ya kihistoria ya ukoloni na biashara ya utumwa ya karne ya 19 pamoja na utamaduni, mila na desturi za wenyeji wa pwani.

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna kambi za jumuiya, binafsi na nyumba za wageni zinazomilikiwa na hifadhi pamoja na watu binafsi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika miji midogo ya Saadani, Gama na Miono.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 689 062 346
Barua pepe: saadani@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 689 062 346
Instagram: saadani_nationalpark

## HIFADHI YA TAIFA

# SERENGETI



### Historia ya Hifadhi



Hifadhi hii ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 1952. Wakati wa kutangazwa kwake, mipaka ilibadilishwa na baadhi ya maeneo kuongezwa mwaka 1952 na hifadhi kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 14,763. Ni sehemu ya mfumo mkubwa wa ikolojia kwenye eneo la kiasi cha kilomita za mraba 35,000. Hifadhi hii ni eneo ambapo *"Uhai wa Dunia Unawezekana Kuwepo"* (Biosphere reserve) na *"Kituo cha Urithi wa Dunia"* (World Heritage Site).

Hifadhi hii ni maarufu duniani kwani ni sehemu ambayo zaidi ya nyumbu milioni moja pamoja na wanyamapori wengine huama kwa msimu, jambo ambalo ni la kuvutia sana duniani. Pia hifadhi hii ndio pekee hupatikana wanyama wakubwa watano ambao ni Tembo, Nyati, Faru, Simba na Chui. Serengeti ndiyo nyumbani na makazi ya makundi makubwa kuliko yote duniani ya Nyumbu, Pundamilia, Mbwamwitu, Pofu, Simba, Duma, Fisi na Swala. Hifadhi hii ina mandhari nzuri yenye kuvutia, hali nzuri ya hali ya hewa ambapo mchana ni jua na joto na usiku wenye baridi.



Hifadhi hii imeshinda tuzo mbalimbali za kiTaifa na kimaTaifa ambapo kwa mara kadhaa imechaguliwa kuwa hifadhi bora zaidi Afrika. Ni pale tu unapoingia katika ardhi ya Serengeti, ndipo pale ukubwa wa eneo lake unapokuwa halisi kwako. Watu wengi hufikiri, ni eneo ambalo unaweza kutembelea kwa siku mbili kabla ya kwenda sehemu nyingine, La-hasha! kuna sehemu tofauti hapa zenye makazi ya wanyama wa aina mbalimbali kuanzia nyanda za wazi, milima hadi misitu.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ipo Kaskazini mwa Tanzania katika mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga na Arusha kwenye wilaya za Serengeti, Tarime, Bunda, Busega, Bariadi, Itilima, Meatu na Ngorongoro.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua katika ambapo mvua za masika huanza kunyesha mwezi Februari hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi inafikika kupitia malango ya Naabi Hill, Seronera, Ndutu, Kusini, Kirawira, Handajega, Ikoma, Tabora B, Lamai na Kleins.

**Kwa anga;** Kuna viwanja vidogo vya ndege vinavyotumika majira yote ya mwaka. Kiwanja cha Seronera kilichopo katikati ya hifadhi, kiwanja cha Kusini kilichopo Kusini mwa hifadhi, Lobo kilichopo Mashariki, Kirawira kilichopo Magharibi na Kogatende na Lamai vilivyopo Kaskazini mwa hifadhi.

## Vivutio vya utalii

- **Makundi makubwa ya wanyama wahamao (Nyumbu na Pundamilia)**; Hifadhi ina nyumbu wahamao kwa makundi makubwa ya wanyama milioni 1.3 au zaidi na pundamilia 300,000. Wanyama hawa huama kila mwaka kufuata misimu ya mwaka ikiwa ni pamoja na wanyama wanaowinda.
- **Idadi kubwa ya wanyama wawindao;** Hifadhi hii ndio hifadhi yenye idadi kubwa ya wanyama wawindao duniani. Wanyama hawa ni kivutio kikubwa unapotembelea hifadhi hii.
- **Serengeti Kopjes;** Hizi ni alama za kipekee kwa Hifadhi ya Taifa Serengeti na mara nyingine wageni huziita *"visiwa kwenye bahari ya nyasi"*. Maeneo haya hutoa makazi wakati wa mioto ya kiangazi, hutunza maji na ni maeneo ya maficho kwa wanyama na pia maeneo yanayowawezesha wanyama wawindao kuweza kuona mbali.
- **Tambarare kubwa;** Tambarare hii ina mandhari nzuri ya asili ambapo wanyama wa aina mbalimbali hupatikana.
- **Maeneo ya tamaduni;** Maneo hayo ni kama vile miamba ya "Ngong rocks", michoro ya kimasai, magofu, minara na mapango yaliyopo Magharibi mwa hifadhi maeneo ya Handajega.

## Shughuli za utalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Kutembelea mbuga kwa kutumia gari. Hii ndiyo shughuli kubwa katika mtandao wa barabara zilizopo kwenye Hifadhi;
- Utalii wa kutembea kwa miguu;
- Utalii wa puto, kwa sasa unawezekana upande wa Kaskazini na katikati mwa Hifadhi;
- Utalii wa kutengeneza filamu;
- Utalii wa kuangalia Faru; na
- Utalii wa kuangalia wanyama wahamao wakiwa wanavuka mito.

## Mtazamo kuhusu safari

Serengeti ipo karibu katika kila orodha ya mgeni anayetaka kuja kutalii Tanzania, lakini mtu anaweza kuifurahia zaidi safari yake ya utalii Tanzania kwa kujumuisha sehemu nyinginezo za Tanzania katika orodha yake kama vile Hifadhi za Taifa Tarangire, Manyara, Kilimajaro na Arusha. Uwepo wa pori kubwa





Kusini na Kaskazini mwa Hifadhi, na mwonekano mzuri wa Ziwa Viktoria unaleta mandhari ya kupendeza. Yote haya yanaifanya hifadhi hii kuwa eneo la kipekee la kutembelea hivyo panga na usikose kutembelea hifadhi hii yenye maajabu mengi.

*Karibu tena siku nyingine!*

Ukiwa Serengeti unaweza kutemebelea Fort Ikoma, ngome ya Kijerumani iliyowekwa mwishoni mwa miaka ya 1890's ili kueneza ushawishi eneo la Kaskazini la Afrika Mashariki. Ngome hiyo iko juu ya sehemu ya Mashariki kabisa ya mlolongo wa vilima vifupi yapata maili moja Kaskazini mwa Mto Grumeti.

Mzungu wa kwanza kukanyaga eneo hili alikuwa Mtafiti wa Kijerumani na mwana mazingira, Dkt. Oscar Baumann, ambaye alipita tu kama Wakala wa Kamati ya Kijerumani ya kupinga ukoloni wakati akielekea Burundi mwaka 1892. Baumann, kimsingi alikuwa mzungu wa kwanza kutembelea Ngorongoro na Serengeti pamoja na washirika wake waliojenga Ngome. Ngome ilikuwa ni kituo cha utawala na ngome ya kijeshi ya Wajerumani mpaka ilipoangukia mikononi mwa Waingereza mwaka 1917 kwani Wajerumani walilazimishwa kurudi nyuma kutoka nchi hii inayoitwa Tanzania kwa sasa wakati wa vita ya kwanza ya dunia.

### "RAMANI YA NJIA MAARUFU ZA UHAMIAJI WA WANYAMA"





Nukuu ya mwanabaolojia maarufu George Schaller

*"Katika kutamani matumaini yetu na kuzitafuta ndoto zetu, tunakipata kile tunachokitafuta Serengeti. Basi walau mara moja katika maisha kila mmoja angetembelea mbuga hii ili akaone maajabu yake na kugundua muda mwingi uliopita bure. Kama ingenipasa kuchagua kituo kimoja duniani, basi ni Serengeti. Huko inaishi mizimu mikali ya watu wa kale, huko wanyama wanatafuta hatima yao, kumbukumbu za nyakati ambapo tulikuwa bado tukitangatanga kabla ya dunia ya kihistoria.*

*Kule kushudia aina fulani ya utulivu wa maisha kunahuisha nafsi zetu na kuturejeshea kujisikia kwamba sisi ni sehemu ya dunia ya asili. Hakuna anayeweza kurudi kutoka Serengeti pasipo kubadililka, kwani wale Simba wenye rangi ya hudhurungi, daima watakuwa katika kumbukumbu zetu na makundi makubwa ya wanyama wanaohama"*

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Kuna kambi za umma, kambi binafsi, kambi za msimu, hosteli, nyumba ya kupumzika wageni, malazi yanayotolewa na makampuni binafsi, hoteli za kimaTaifa na kambi za kudumu.



Pia kuna maeneo ya kupiga mahema na nyumba za wageni karibu na lango la kuingilia hifadhini

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika miji midogo ya Mugumu, Musoma na jiji la Mwanza.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 282 985 619
Barua pepe: serengeti@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 689 062 243
Instagram: serengeti_national_park

# HIFADHI YA TAIFA TARANGIRE



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Tarangire ilianzishwa mwaka 1970 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 2,600. Hifadhi hii ni sehemu ya mfumo wa ikolojia wa Manyara - Tarangire. Sehemu kubwa ya mfumo huu ni uwanda wa Maasai. Hifadhi hii ina mandhari nzuri iliyopambwa na maeneo makubwa ya wazi, uoto wa savana, mibuyu, mito yenye mchanga, wanyama, ndege na wadudu wa aina mbalimbali. Mto Trangire ndio mto pekee wa kudumu unaopita ndani ya hifadhi na ndio kimbilio la wanyama wakati wa majira ya kiangazi.

## Mahali ilipo

Hifadhi ipo katika mikoa ya Arusha, Manyara na Dodoma kwenye wilaya za Monduli, Kondoa, Babati vijijini, Simanjiro na Kiteto.

## Hali ya hewa

Hifadhi hii ina misimu miwili ya mvua ambapo mvua za vuli huanza kunyesha mwezi Novemba hadi Desemba na mvua za masika huanza kunyesha mwezi Machi hadi Mei. Kipindi cha kiangazi huanza mwezi Juni mpaka Oktoba na Januari hadi Februari.

## Jinsi ya kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Hifadhi hii inafikika kwa njia ya barabara umbali wa kilomita 121 kutoka jiji la Arusha na kilomita 160 kutoka uwanja wa ndege wa kimaTaifa wa Kilimanjaro. Pia hifadhi inafikika kutoka Dodoma umbali wa kilomita 338.

**Kwa anga;** Kwa kutumia ndege za kukodi na kutua katika uwanja mdogo wa ndege, Kuro uliopo ndani ya hifadhi. Pia kwa kutumia uwanja wa Arusha na uwanja wa kimaTaifa wa Kilimanjaro.

## Vivutio vya utalii

- **Wanyamapori;** Hifadhi hii ni maarufu kwa kuwa na makundi makubwa ya Tembo kuliko hifadhi nyingine nchini Tanzania. Wanyama wanaopatikana kwa wingi mbali na Tembo ni Simba, Chui, Duma, Fisi, Mbweha, Mbwamwitu, Twiga, Pundamilia, Nyati, Kongoni na Nyani. Pia hifadhi hii ni maarufu kwa kuwepo kwa aina ya Chatu walio na uwezo wa kupanda miti.
- **Mimea – Mibuyu;** Hifadhi hii ni maarufu kwa kuwa na miti mikubwa aina ya Mibuyu. Mibuyu hii ina maumbile ya kipekee na huweza kuwa na shina lenye kipenyo cha futi mia moja. Uwepo wa miti hii unaongeza uzuri na mandhari ya uoto wa asili.
- **Mto Tarangire;** Mto huu umepita katikati ya Hifadhi na hupata maji yake toka ardhi oevu za Silale na Lamakau ambazo hutunza maji mengi wakati wa misimu ya mvua. Mto huu ni chanzo cha maji kwa





wanyama waliopo hifadhini hasa wakati wa kiangazi, jambo linalolifanya eneo hili liwe la kuvutia kutokana na kuwepo kwa aina nyingi za wanyama.

- **Ndege;** Hifadhi hii ina zaidi ya aina 500 za ndege wanaofanya makazi yao kwenye nchi kavu na ardhi oevu. Uwepo wa ndege hawa huifanya hifadhi hii kuwa maarufu kwa watalii wanaopenda kufanya utalii wa ndege. Wakati mzuri zaidi wa utalii wa ndege ni masika ambapo ndege wengi huzaliana na kuwa na manyoya yenye rangi za kuvutia.
- **Kuwepo kwa vichuguu;** Vichuguu hivi vilivyojengwa kwa tope lililochanganywa na mate ya Mchwa vimekuwa kama makazi ya wanyama wawindao na wawindwao, kuweza kuangalia na kuona mbali. Pia ni makazi ya baadhi ya wanyama kama Vicheche na sehemu ya kujipatia chakula kwa wanyama walao mchwa kama Mhanga na Kakakuona.

## Shughuli za Utalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa wa kuona wanyama kwa gari. Utalii huu hufanyika kwa kuangalia wanyama wakati ukiwa ndani ya gari. Mtalii atapata fursa ya kuona wanyama kama Simba, Chui, Duma, Fisi, Tembo, Nyati, Twiga, Nyumbu, Pundamilia na Chatu wapandao miti;
- Utalii wa kutembea kwa miguu. Aina hii ya utalii inakuongezea fursa ya kuona na kujifunza zaidi tabia mbalimbali za wanyama kwani unamwezesha mgeni kuwa karibu kabisa na mazingira ya hifadhi;
- Utalii wa kuruka kwa puto. Aina hii ya utalii unakupa kionjo tofauti kabisa wakati unapopita juu ya mto Tarangire huku nyika na nyasi zikiwa zimekolezwa rangi za pinki na dhahabu zinasosababishwa na mawio ya jua. Pia utalii huu unamwezesha mgeni kuona makundi makubwa ya wanyama tokea angani;
- Kutazama ndege; Hifadhi hii ni nzuri kwa utalii wa kutazama ndege kwani ina jumla ya aina 500 za ndege; na
- Utalii wa kuona wanyama kwa gari usiku. Utalii huu hufanyika muda wa usiku kwa hutumia gari la wazi. Utaliii huu utakuwezesha kujionea wanyama wawindao nyakati za usiku kama vile Chui, Simba na Pakapori.

## Huduma za Malazi

**Ndani ya hifadhi;** Hifadhi ina nyumba za kulala wageni na kambi za kupiga mahema. Pia zipo loji ambazo zinamilikiwa na watu binafsi.

**Nje ya hifadhi;** Kuna aina mbalimbali za malazi nje ya hifadhi katika miji ya Babati na Makuyuni.

**Mawasiliano:**
Simu: +255 689 062 248
Barua pepe: tnp@tanznaiaparks.go.tz
Whatsapp: +255 689 062 248
Instagram: tarangire_national_park

# HIFADHI YA TAIFA
# ZIWA MANYARA



## Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara ilitangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 1960 na kuandikishwa na Umoja wa MaTaifa kama *"Usitiri wa Maisha"* mnamo mwaka 1981 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 649. Kati ya hizo ziwa linachukua eneo la kilomita za mraba 263 na nchi kavu kilomita za mraba 386.

Unapoanza kuingia hifadhini utakutana na uoto wa msitu wa asili wa maji ya ardhini wenye miti mirefu ambayo ni makazi ya makundi ya Nyani na Kima. Baada ya msitu huu utakutana na msitu wa migunga, vichaka, mbuga za nyasi fupi na tindiga. Hifadhi ina maelfu ya ndege aina ya Heroe wadogo pamoja na ndege wengine wahamao kutoka sehemu mbalimbali za mabara ya Afrika, Asia na Ulaya. Ziwa hili lina sifa ya kuwa na magadi ambapo mimea aina ya mwani wa bluu-kijani humea na ndicho chakula kikuu cha Heroe wadogo.

## Mahali ilipo

Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara ipo Kaskazini mwa Tanzania katika Mikoa ya Arusha na Manyara kwenye wilaya za Monduli, Karatu, Babati na Mbulu.

## Hali ya hewa

Kuna misimu miwili ya mvua ambapo mvua za masika huanza kunyesha kuanzia mwezi Februari hadi Mei na mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Desemba. Msimu wa kiangazi huanza mwezi Juni hadi Oktoba.

## Jinsi ya Kufika

Hifadhi inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa barabara;** Barabara ya Makuyuni – Ngorongoro kilometa 115 kutoka jiji la Arusha karibu na mji mdogo wa Mto wa Mbu.

**Kwa anga;** Kwa kutumia uwanja wa ndege wa KimaTaifa wa Kilimanjaro au uwanja mdogo wa Arusha. Pia kwa kutumia uwanja mdogo wa ndege wa Manyara ambao una ratiba za kawaida za ndege (wakati wa mchana) kwa kipindi cha mwaka mzima.

## Vivutio vya utalii

- **Simba wakweao miti;** Eneo la msitu wa migunga ndio eneo linalopendwa zaidi na Simba hawa wapandao miti. Inaaminika kwamba moja ya sababu za Simba kupanda miti ni kuona mawindo yaliyo mbali na pia kuondokana na usumbufu wa wadudu kama Inzi na Mbung'o.
- **Ziwa Manyara;** Ziwa lenye mandhari ya kupendeza na makazi ya makundi makubwa ya ndege aina ya Heroe wadogo
- **Chemichemi ya maji moto;** Hifadhi ya Ziwa Manyara ni maarufu kwa kuwa na chemchemi za majimoto. Maji hayo huchemka na kufikia jotoridi la sentigradi



40 – 76.50. Kuna zaidi ya chemchemi kumi na tano katika eneo la kilometa mbili. Maji haya yana madini mbalimbali ikiwemo "Sulphur "ambayo hutumika kutibu magonjwa ya ngozi na pia hutoa mazingira mazuri kwa kutengenezwa chakula cha Heroe wadogo.

- **Msitu wa maji ya ardhini;** Msitu uliofunga wa kijani kibichi kwa kipindi chote cha mwaka, hulishwa na chemichemi na vijito vinavopita chini kwa chini kutoka ukuta wa bonde la ufa. Msitu huu ni makazi ya wanyama kama Kima, Nyani, Pongo na ndege wa msituni.
- **Wanyama;** Eneo hili lina aina nyingi za wanyama na makazi ndani ya eneo dogo
- **Msitu mnene wa Marang';** Msitu huu upo ukanda wa juu katika miteremko ya ukuta wa bonde la ufa. Msitu wa Marang ni makazi ya jamii mbalimbali za wanyama kama vile Tembo, Nyati, Nyani, Kima na Swala wadogo. Jamii za ndege wa msituni ni kama Hondo hondo, Tai, Mwewe na pia kuna jamii za miti kama Mtakahiko, Loliondo, Mfuruanji na Mkuyu.
- **Ndege;** Hifadhi ina aina mbalimbali za ndege (zaidi ya aina 400) wahamao na wakazi.
- **Bwawa la viboko;** Bwawa hili linatoa fursa kwa wageni kuweza kujionea viboko kwa urahisi.
- **Ukuta wa Bonde la Ufa;** Ukuta wa bonde la ufa ambao hugawanya eneo la juu na la chini la hifadhi hutoa madhari nzuri ya hifadhi.

## Shughuli za Kitalii

Shughuli kuu za kitalii ni pamoja na;

- Utalii wa kutwa kwa kutumia magari. Hii ndiyo shughuli kubwa katika mtandao wa barabara zilizopo kwenye Hifadhi;
- Kupanda milima. Kutembea kwenye mlima wa Marang kupitia Mto Lyambi uliopo Kusini mwa hifadhi;
- Utalii wa kuangalia wanyama usiku. Utalii huu hufanyika kwa kutumia magari maalum na kuweza kuona wanyama watembeao usiku;
- Kuendesha mitumbwi. Uendeshaji mitumbwi kutegemea na kina cha maji ziwani;
- Utalii wa kula chakula cha moto hifadhini. Aina hii ya utalii unawezesha mtalii kupata nafasi ya kula chakula cha moto akiwa porini huku akifurahia kuona wanayama na ndege mbalimbali;
- Utalii wa kutazama Ndege. Hifadhi hii ni makazi ya aina za ndege zaidi ya 400 ambao wana makazi ya kudumu na wengine ni wahamaji. Mtalii anaweza kuona aina za ndege zaidi ya 100 kwa siku; na
- Kutembea juu ya daraja la kamba ambalo ni la kipekee kabisa kwa Hifadhi za Taifa. Daraja hili linatoa fursa ya kipekee ya kutizama wanyamapori na ndege mbalimbali kutokea juu ya miti.

## Huduma za Malazi


**Ndani ya hifadhi;** Kuna maeneo ya kupiga mahema na nyumba za wageni karibu na lango la kuingilia hifadhini

**Nje ya hifadhi;** Kuna nyumba za kulala wageni katika mji mdogo wa Mto wa Mbu na Karatu.

**Mawasiliano:**

Simu: +255 232 935 036
Barua pepe: manyara@tanzaniaparks.go.tz
Whatsapp: +255 767 536 137
Instagram: lake_manyara_national_park

# Ilani ya Arusha



"Uhai wa wanyamapori wetu ni jambo la muhimu sana kwetu sisi sote Afrika. Hawa viumbe-pori pamoja na mazingira-pori wanayoishi si tu ni muhimu kwa sababu ni chanzo cha maajabu na kuvutia bali hivi ni vitu muhimu katika rasilimali zetu za asili na kwa mustakhabali wa maisha yetu na ustawi wetu.

Katika kukubali udhamini wa wanyamapori wetu, tunatangaza kwa dhati kwamba tutafanya kila kitu kilicho ndani ya uwezo wetu ili kuhakikisha kwamba vitukuu vinaufurahia utajiri na urithi huu wenye thamani kubwa.

Uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yenye mapori unahitaji maarifa ya kitaalamu, nguvu kazi yenye mafunzo, na fedha, na tunatarajia maTaifa mengine kushirikiana pamoja nasi katika kazi hii muhimu - ambayo mafaniko yake au kushindwa kwake si tu kwamba kunaliathiri bara la Afrika bali dunia nzima

JK Nyerere, 1961

# Wajibu wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa





### Wajibu wa msingi

Wajibu wa msingi wa Hifadhi za Taifa ni uhifadhi. Hifadhi za Taifa 22 ambazo nyingi katika hizi ndizo kiini cha sehemu kubwa ya mfumo wa ikolojia inayolindwa, zimetengwa kwa ajili ya kutunza urithi wa asili wa nchi na kutoa mazingira mazuri ya kuzaliana ambapo mimea na wanyama wake vinaweza kustawi, na kuwa salama dhidi ya mgongano wa maslahi unaotokana na idadi ya watu inayozidi kuongezeka.

### Ulinzi wa rasilimali za hifadhi, huduma na wageni

Ni wajibu wa TANAPA kuhakikisha ulinzi na usalama wa wageni, hifadhi na wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi. Ingawa ulinzi ni wajibu wa kila mkazi anayeishi ndani ya hifadhi, taasisi inao waangalizi wa hifadhi ambao wanahusika moja kwa moja katika hili. Ili kuhakikisha kwamba waangalizi wana stadi za kutosha kutekeleza majukumu yao, aina mbalimbali za mafunzo yanaendeshwa na vifaa vinatolewa kurahisisha utendaji.

### Ufuatiliaji na usimamizi wa afya ya mfumo wa ikolojia

Hifadhi za Taifa zimejaliwa utajiri na aina mbalimbali wa mazingira pamoja na mifumo ya ikolojia ambayo inasaidia aina mbalimbali za makundi ya wanyama. Ufuatiliaji wa kawaida wa mifumo hii ya ikolojia









unafanyika ili kuweza kuwa na tahadhari za mapema kuhusu matukio ya baadaye. Vipimo ya hali ya hewa vinafuatiliwa katika hifadhi zote kwa mwaka mzima. Sensa za wanyama zinafanyika kama kawaida, ili kuhakiki idadi, mwenendo na jinsi makundi yalivyo sambaa. Kaguzi za kawaida za mazingira zinafanyika kwenye huduma za wageni na mapendekezo yanayotelewa kuhusu kuboresha mapungufu yanafanyiwa kazi. Miradi yote ya maendeleo inayofanyika katika Hifadhi inazingatia tafiti kuhusu tathmini za athari za mazingira. Afya za wanyamapori katika hifadhi zote inafuatiliwa kwa karibu sana. Orodha, ubainishaji katika ramani na utokomezaji wa spishi zisizo za kawaida unafanyika katika maeneo yaliyoathirika.

Uchomaji moto wa mapema hufanyika ili kukabiliana na athari za mioto ya kiangazi ili kutunza chakula cha wanyama walao majani. Hii hufanikishwa kupitia uchomaji wa mpangilio na kuacha baadhi ya maeneo wakati wa uchomaji wa mapema. Tafiti zinazohusiana na wanyamapori katika hifadhi zinahimizwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI).

### Msaada kwa jamii na elimu ya uhifadhi

Njia mbalimbali zinatumika kutoa elimu ya uhifadhi kwa wadau mbalimbali wa uhifadhi.

Tasisi hutoa msaada wa kifedha kwa vijiji 1,132 vinavyopakana na Hifadhi za Taifa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii kupitia Mpango wa Msaada kwa ajili ya Miradi Iliyoanzishwa na Jamii (SCIP). Miradi hii inalenga katika elimu, afya, usafirishaji na usambazaji wa maji.

### Mchango kwa ajili ya washirika wa uhifadhi

Taasisi inatambua wajibu unaofanywa na tasisi zilizopo ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na nyinginezo katika kusaidia kufanikisha majukumu yake. .

### Maendeleo ya Utalii na Uhamasishaji

TANAPA inaedelea kutambua utalii kama chanzo chake cha mapato kwa ajili ya uedeshaji wa shughuli zake. Na kwa sababu hiyo, itaendelea kuhakikisha kwamba bidhaa zaidi za utalii na shughuli zake vinaendelezwa na kuhamasisha unyumbulishaji wa uzoefu wa utalii katika hifadhi.

Ikiwa kama mkakati mojawapo wa kujinadi, taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine, inaedelea kukuza vivutio vya utalii vya nchi, kiTaifa na kimaTaifa. Maendeleo ya huduma za utalii kwenye hifadhi na katika mazingira yanayozizunguka ni jambo linalosisitizwa pia.



# Usalama ndani ya hifadhi



## Utalii wa magari

- Usizidishe mwendo wa gari zaidi ya kiwango kilichowekwa;
- Usiendeshe gari nje ya barabara. Fuata alama zilizowekwa;
- Usiwasogelee wanyamapori zaidi ya umbali uliowekwa; na
- Usipige kelele na epuka sauti kubwa pamoja na muziki.



## Kuweka kambi

- Ifanyike kwenye vituo vilivyo ainaishwa tu; na
- Uwe na tahadhari.



## Uendeshaji mitumbwi au usafiri kwenye maji

- Siku zote beba jaketi okozi; na
- Fuata maelekezo ya mwongozaji/kapteni



## Upandaji Milima

- Siku zote msikilize mwongoza mgeni wako; usikose kumwona muda wote;
- Panda taratibu ili kuepuke magonjwa ya mlima;
- Kunywa maji ya kutosha; na
- Watoto wenye umri chini ya miaka 10 hawaruhusiwi kupanda zaidi ya mita 3700 toka usawa wa bahari.



## Kutembea daraja la juu ya miti

- Usizidishe idadi ya wageni iliyopendekezwa; na
- Tembea kwa uangalifu.



## Utalii wa kutembea kwa miguu

- Ufanyike kwenye njia zilizopendekezwa tu; na
- Ambatana na mwangalizi mwenye silaha.



## Matembezi ya kuwaona Sokwemtu

- Kama unaumwa, haurusiwi kufanya matembezi haya;
- Watoto chini ya umri wa miaka 12 hawaruhusiwi kufanya zoezi hili; na
- Lazima uambatane na mwogoza wageni muda wote.





## *Wito wa Afrika*

C Emily-Dibb

*Baada ya kuwa umeonja ladha ya vumbi,*
*harufu ya mvua yetu ya kwanza,*
*tayari utakuwa umeshikamanishwa*
*na Afrika maisha yako yote,*
*Na hutakuwa sawa tena*
*Mpaka utakapoweza kuuona mwezi ukizama*
*Na ukasikia mibweko ya Bweha*
*Na sasa utatambua ya kwamba wapo karibu*
*nawe wakisubiri gizani.*

*Wakati ukiwa na shauku ya kuwaona tembo,*
*Au kusikia wimbo wa ndege,*


*Mwezi unapochomoza damu yako inachemka,*
*Umekuwa mbali kwa muda mrefu sana.*
*Muda umefika wa kujiachia na kufurahia maisha*
*Na kuuachia moyo wako uwe huru*
*Kupita huo upeo wa macho,*
*Huko ambako moyo wako unatamani kuwa.*

*Afrika inasubiri…njoo!*
*Kwa kuwa umeligusa anga angavu*
*Na kujifunza  kupenda majani yanayotoa*
*sauti ya mrudiorudio*

*Kilio cha tai,*
*Daima utakuwa na jaa ya pori,*
*Kwa muungurumo wa simba,*
*Kuweka kambi, walau chini ya nyota*
*Na kuwa na amani kwa mara nyingine tena.*

# Historia fupi ya TANAPA

Mwanzoni mwa uhuru mwaka 1960 Tanzania ilikuwa na Hifadhi ya Taifa moja tu ya Serengeti. Nchi nyingine za Afrika zilionesha kutokujali uhifadhi wa wanyamapori sawasawa na walivyofanya watawala wao wa kikoloni wa zamani, hivyo mnamo Septemba 1961 IUCN na wakala nyinginezo za uhifadhi walifanya mkutano  Arusha ili kuzungumzia suala zima la uhifadhi.



*Rais Mwl. Julius Nyerere, 1965*


Mkutano huo ulihudhuriwa na wataalamu wengi na watu mashuhuri akiwemo Rais wa Kwanza wa Tanzania Mwl. Julius K. Nyerere na mwanabiolojia maarufu, Sir. Julian Huxley, Chifu Fundikira (Waziri wa Sheria) ambae alikuwa Mwenyekiti.

Taswira ya kikao ilionekana baada ya Chifu Fundikira kuwasilisha Ilani ya Arusha kwa niaba ya rais. Wajumbe waliipokea ilani kwa makofi mengi, na Sir. Julian Huxley akatangaza "Hii ni alama kwa Afrika, alama ya jumla kwa dunia nzima, na kwakweli ni alama kwa uhifadhi wa asili".



*Chifu Fundikira*

Rais Mwl. Julius K. Nyerere alikuwa tu ndiye aliyemteua Dkt. John Owen (mtu mweupe), kuwa Mkurugenzi wa kwanza kusimamia Hifadhi za Taifa Tanzania, na Rais alimpa mamlaka ya kuongeza Hifadhi za Taifa  mpaka zifike kumi. Watu hawa wakawa marafiki wazuri na mpaka wakati Dkt. John Owen anastaafu kutoka kwenye nafasi yake mwaka 1970 Tanzania ilikuwa na Hifadhi za Taifa kumi. Rais alikuwa amemwomba Dkt. John Owen kuendelea kama Mkurugenzi wa Hifadhi za Taifa, lakini hakuwa tayari  akiamini ya kwamba msingi wa kutosha ulikuwa tayari umewekwa kwa ajili ya watanzania kushika hatamu.



*Dkt. John Owen*

Tokea siku hizo za mwanzo, Tanzania imeendeleza dira yake ya kutunza maeneo-pori yake na wanyamapori wa maeneo hayo kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vya baadaye, na kwa sasa kuna Hifadhi za Taifa 22.



*William S. Mwakilema*

Chini ya uongozi wa Kamishna wa Uhifadhi, William S. Mwakilema, TANAPA sasa inasimamia shughuli zake kwa kuzingatia viwango vya ubora wa kimataifa. Hivyo, kuifanya Taasisi hii kuwa mojawapo ya nguzo muhimu za uchumi wa Taifa.

# MAWASILIANO YA HIFADHI ZA TAIFA

**ARUSHA**
S. L.P. 3134, Arusha
**Simu:** +255 689 262 363
**Barua pepe:** arusha@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** arusha_nationalpark

**BURIGI-CHATO**
S. L. P. 444 Karagwe, Kagera
**Simu:** +255 282 983 204
**Barua pepe:** bc@tanzaniapark.go.tz
**Instagram:** burigichato_national_park

**GOMBE**
S. L. P. 185, Kigoma
**Simu:** +255 282 988 228/229
**Hotline:** +255 689 062 303
**Barua pepe:** chimps@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** gombe.nationalpark

**IBANDA-KYERWA**
S. L. P. 147, Karagwe
**Barua pepe:** ibandakyerwa@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** ibandakyerwa_national_park

**KATAVI**
S. L. P. 89, Mpanda
**Hotline:** +255 767 536 128
**Barua pepe:** katavi@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** katavipark

**KIGOSI**
S. L. P. 80, Masumbwe-Mbogwe
**Barua pepe:** kigosi@tanzaniaparks.go.tz

**KILIMANJARO**
S. L. P. 96, Marangu
**Simu:** +255 272 974 153
**Hotline:** +255 739 767 679
**Barua pepe:** kinapa@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** mountkilimanjaro_national_park

**KITULO**
S. L. P. 1965, Mbeya
**Simu:** +255 262 698 984
**Hotline:** +255 767 536 130
**Barua pepe:** kitulonp@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** kitulo_national_park

**ZIWA MANYARA**
S. L. P. 12, Mto wa Mbu
**Hotline:** +255 767 536 137
**Barua pepe:** manyara@tanzaniaparks.go.tz
Instagram: lake_manyara_national_park

**MILIMA YA MAHALE**
S. L. P. 1374, Kigoma
**Simu:** 255 282 988 244
**Barua pepe:** sokwe@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** mahaletourism

**MIKUMI**
S. L. P. 62, Mikumi
**Simu:** +255 767 536 135
**Hotline:** +255 733 670 879
**Barua pepe:** mikumi@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** mmikumi_nationalpark

**MKOMAZI**
S. L. P. 41, Same
**Simu: +255 27 297 4165**
**Hotline:+255 624 333 888**
**Barua pepe:** mkomazi@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** mkomazi_park_tanzania

**NYERERE**
S. L. P. 468, Morogoro
**Simu:** +255 232 935 351
**Hotline Tourism:** +255 762 012 700
**Barua pepe:** nyerere@tanzaniaparks.go.tz
Instagram: nyerere_national_park

**RUAHA**
S. L. P. 369, Iringa
**Simu:** +255 262 968 972 / 964
**Booking:** +255 756 144 400
**Barua pepe:** ruaha@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** ruaha_national_park

**RUBONDO ISLAND**
S. L. P. 111, Geita -Nkome Gate
**Simu:** +255 282 893 184
**Barua pepe:** sitatunga@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** rubondoisland_tz

**RUMANYIKA-KARAGWE**
S. L.P. 147, Karagwe
**Barua pepe:** ir@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** rumanyikakaragwe_national_park

**SAADANI**
S. L. P. 133, Pangani
**Simu:** +255 232 935 036
**Hotline:** +255 689 062 346
**Barua pepe:** saadani@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** saadani_nationalpark

**KISIWA CHA SAANANE**
S. L. P. 11775, Mwanza
**Simu:** +255 282 541 819
**Hotline:** +255 689 062 276 / 767 536 139
**Barua pepe:** saanane@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** saananeisland_national_park

**SERENGETI**
S. L. P. 3134, Arusha
**Simu:** +255 282 985 619
**Hotline:** +255 689 062 243
**Barua pepe:** serengeti@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** serengeti_national_park

**TARANGIRE**
S. L. P. 3134, Arusha
**Simu:** +255 689 062 248
**Barua pepe:** tnp@tanznaiaparks.go.tz
**Instagram:** tarangire_national_park

**MILIMA YA UDZUNGWA**
S. L. P. 99, Mang'ula
**Simu:** +255 232 934 316
**Barua pepe:** udzungwa@tanzaniaparks.go.tz
**Instagram:** udzungwamountain_national_park

**MTO UGALLA**
S. L. P. 08, Kaliua-Tabora
**Barua pepe:** ugalla@tanzaniaprks.go.tz

# RAMANI YA HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA






# Kuhusu Tanzania





### KWELI & TARAKIMU

**Ni nchi iliyoko Afrika Mashariki**

**Ukubwa (Nchi kavu & maji) 947,300 km²**

**Idadi ya Watu (Makadirio ya 2022) 61,741,120**

**Kipato cha kila mtu (Makadirio ya 2016) US $ 3,100**

# Dondoo kuhusu safari

## Maandalizi ya safari

Chagua hifadhi unayotaka kuitembelea, andaa bajeti kutokana na chaguzi zako kwa kuzingatia aina ya usafiri, malazi, chakula na tozo za hifadhi.

## Usafiri

Andaa usafiri wako au tumia wakala wa utalii.

## Malazi

Baadhi ya Hifadhi za Taifa zina maeneo ya malazi ya bei nafuu, wasiliana na wahusika kwa ajili ya kupata taarifa na kuweka nafasi.

## Chakula

Huduma ya chakula inapatikana kwa kutoa taarifa mapema, pia kwa anaependa kujiandalia chakula mwenyewe, baadhi ya hifadhi zinatoa maeneo kwa ajili ya huduma hii.

## Mavazi

Zingatia mavazi stahiki kulingana na hali ya hewa na mazingira ya hifadhi. Ukipenda unaweza kubeba kofia na miwani ya jua.

## Malipo

Lipa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki wa TANAPA mfumo wa kadi za kielektroniki na mitandao ya simu. Tozo hizi hulipwa wakati wa kuingia hifadhini.

**NB: "Fanya malipo ya kuwekewa nafasi au kulipia kabisa kupitia mifumo ya mtandao wa TANAPA kwa kutumia kadi ya kielektroniki"**

- Gharama hizi hazijumuishi VAT 18%.
- Tozo zote zinatumika mara moja tu kuingia na muda wa matumizi unadumu kwa muda wa masaa 12 au 24.
- Wale wenye Vibali vya Wakurugenzi/Meneja wa Kambi hawaruhusiwi kuambatana na wageni.
- Ada ya kiingilio hulipwa kabla ya kuingia hifadhini.

MasterCard VISA Bank Teller



## Uhifadhi Endelevu kwa ajili ya Maendeleo

KAMISHNA WA UHIFADHI
HIFADHI ZA Taifa TANZANIA
JENGO LA TANAPA
BARABARA YA DODOMA
S. L. P. 3134
ARUSHA - TANZANIA

SIMU: +255 (27) 297 0404
+255 (27) 297 0405
NUKUSHI: +255 (27) 297 0408
info@tanzaniaparks.go.tz
www.tanzaniaparks.go.tz

*Matini*
*Tim Corfield*

*Usanifu*
*Meja Graphics (T) Limited*

Hatimilliki 2020
Hifadhi za Taifa Tanzania

*Tafadhali pakua kipeperushi chetu*